# MAUDHUI YA UADILIFU KATIKA NYIMBO ZA JOSEPH NGALA

**NA**

**EVALINE K. KANYANGE**
**(C50/84016/2012)**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2015**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asili na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu kingine chochote.

**Sahihi** **Tarehe**

____________________ ______________________

EVALINE K. KANYANGE (Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wateuliwa wa Chuo Kikuu Cha Nairobi.

**Sahihi** **Tarehe**

____________________ ______________________

Prof. Rayya Timammy.

**Sahihi** **Tarehe**

____________________ ______________________

Dkt. Jefwa Mweri.

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mamangu mpendwa Alice Muthoni Kanyange na babangu Joel Njiru Kanyange kwa juhudi zao za kunilea, kunielimisha na kunitia moyo maishani. Tabaruku nyingine ni kwa kakangu William Nyaga kwa kunipa hamasa kila mara ya kumaliza utafiti huu. Hatimaye ni kwa dadangu mpendwa Caroline Karimi kwa kuniunga mkono wakati wa kipindi kigumu nilipokuwa nikiendelea na masomo.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na uwezo wa kukamilisha shahada hii ya uzamili katika somo la Kiswahili.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Rayya Timammy na Dkt. Jefwa Mweri kwa kuwa na subira nami katika kunipa ushauri wenye busara katika utafiti huu. Nawashukuru kwani hawakuchoka kamwe katika kunirekebisha wakati nilikuwa natapatapa katika bahari hii ya usomi. Mola awajalie baraka tele.

Nawashukuru pia wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kwa ushauri walionipa ulioniwezesha kufanya utafiti. Shukrani maalum ziwaendee wahadhiri wafuatao: Prof. Kineene Wa Mutiso aliyenifaa sana katika kupata tatizo la utafiti. Dkt. Iribe Mwangi kwa mihadhara yake iliyochochea fikra zetu ili kujua namna ya kupiga hatua mbele katika usomi huu. Wahadhiri wengine ni pamoja na Prof. John Habwe, Dkt. Ayubu Mukhwana, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Zaja Omboga na Dkt. E. M. Mbuthia.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu wote ambao tulisaidiana nao sana kupitia mijadala mbalimbali na kutiana moyo hasa wakati tulipokumbana na mawimbi makali katika usomi na utafiti. Shukrani maalum ziwaendee Edward Zani, Julita Wanjala, Mutahi Miricho, Flora Omosa na Paul Sito kwa kunitia moyo wakati wa utafiti.

Nawashukuru wazazi wangu Alice Muthoni na Joel Kanyange kwa kujitolea kunielimisha na kuungana nami katika hali yoyote ile niliyokumbana nayo katika utafiti. Vilevile nawashukuru ndugu zangu Josphat Mucangi, William Nyaga, Martin Njeru na Caroline Karimi kwa kunifaa kwa njia moja au nyingine.

Hatimaye namshukuru mwajiri wangu Dkt/Fr. Bill Fryda kwa kukubali kunipa nafasi ya kujiendeleza kielimu.

## IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulikia maudhui ya uadilifu katika nyimbo tulizoteua tisa za Joseph Ngala ambazo ni *Fuateni mambo ya sheria*, *Mwana Mpotevu*, *Ndivyo Ilivyo dunia*, *Nisikilize Mwanangu*, *Ndugu Tupendane*, *Dada Vumilia*, *Simba*, *Kisulisuli* na *Jembe*. Tulilenga kubainisha matendo adilifu yanayojitokeza katika nyimbo hizi, kutoa sababu thabiti za kuainisha matendo hayo kama adilifu kwa kutumia nadharia ya unufaishaji hasi kisha tulieleza matendo hayo yanatoa athari zipi kwa walengwa ambao ni jamii/ mtu binafsi. Matokeo ya utafiti wetu yalidhihirisha bayana kuwa msanii Joseph Ngala ameangazia pakubwa maudhui ya uadilifu katika nyimbo zake ambayo ni pamoja na kutii sheria, kutokuwa na tamaa, kusikiliza mawaidha kutoka kwa wakuu, upendo, uvumilivu, shukrani, ushirikiano na uwajibikaji. Aidha, tulibainisha kuwa matendo haya yanatoa athari chanya kwa jamii/ mtu binafsi.

# YALIYOMO

## SURA YA KWANZA: MAMBO YA KIMSINGI YA UTAFITI


1.0 Utangulizi ..... 1
1.1 Tatizo la utafiti ..... 2
1.2 Maswali ya utafiti ..... 3
1.3 Malengo ya utafiti ..... 3
1.4 Sababu za kuchagua mada ya utafiti ..... 3
1.5 Upeo na mipaka ..... 4
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti ..... 5
1.6.1 Yaliyoandikwa kuhusu nyimbo kwa jumla ..... 5
1.6.2 Yaliyoandikwa kuhusu aina maalum za nyimbo ..... 7
1.7 Msingi wa nadharia ..... 10
1.8 Mbinu za utafiti ..... 12
1.8.1 Mahali pa utafiti ..... 12
1.8.2 Uteuzi wa sampuli ..... 13
1.8.3 Ukusanyaji wa data ..... 13
1.8.4 Uchanganuzi wa data ..... 13
1.8.5 Uwasilishaji wa data ..... 13
1.9 Hitimisho ..... 14


## SURA YA PILI: HISTORIA FUPI YA JOSEPH NGALA NA MTINDO WA NYIMBO ZA BANGO


2.0 Utangulizi ..... 15
2.1 Historia ya Joseph Ngala ..... 15
2.2 Asili ya mtindo wa nyimbo za bango ..... 16
2.3 Dhana ya uadilifu ..... 17
2.4 Maelezo ya nyimbo ..... 23
2.5 Hitimisho ..... 27

**SURA YA TATU: MAUDHUI YA UADILIFU KATIKA NYIMBO ZA JOSEPH NGALA**

3.0 Utangulizi ........ 28
3.1 Kutii sheria ........ 28
3.2 Kutokuwa na tamaa ........ 33
3.3 Kusikiliza mawaidha ya wakuu ........ 38
3.4 Upendo ........ 45
3.5 Uvumilivu ........ 48
3.6 Shukrani ........ 51
3.7 Ushirikiano ........ 54
3.8 Uwajibikaji ........ 57
3.9 Hitimisho ........ 61

**SURA YA NNE: HITIMISHO**

4.0 Utangulizi ........ 62
4.1 Muhtasari wa utafiti ........ 62
4.2 Muhtasari wa matokeo ........ 63
4.3 Changamoto za utafiti ........ 66
4.4 Mapendekezo ........ 66
4.5 Marejeleo ........ 67

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Utafiti tuliofanya ulilenga kuangazia suala la uadilifu katika nyimbo za Joseph Ngala ambaye ni msanii anayejulikana sana pwani mwa Kenya kwa mtindo wake wa nyimbo zijulikanazo kama bango. Uadilifu ni mojawapo ya maudhui anayoangazia katika nyimbo zake.

Nyimbo ni utanzu wa ushairi unaopatikana katika fasihi simulizi na ambao huchukua nafasi kuu katika jamii. Utanzu huu umepewa fasili nyingi ikiwemo:

> Nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka ambapo nyimbo hizi huundwa kwa lugha ya mvuto, matumizi ya taswira na mapigo ya silabi. (Wamitila: 2003:107)

Katika utafiti wetu, tulichukulia kuwa nyimbo ni zaidi ya sauti tu ambazo huimbwa na kuchezwa, kwani nyimbo huwasilisha mambo mbalimbali yenye umuhimu katika jamii husika. Sanaa ya nyimbo huonyesha uwezo wa binadamu wa kusimulia au kupasha tajriba yake na ya jamii ya kila siku na kujaribu kuleta maana katika maisha.

Nyimbo ni utanzu ambao ni rahisi sana kunata makini ya hadhira, na ambao huwafikia watu wengi zaidi katika jamii; hasa nyimbo zinazoimbwa kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya, kwani hueleweka na watu wengi. Hili hufanikisha nyimbo kutekeleza majukumu mengi katika jamii ambayo ni pamoja na kuelimisha kuhusu masuala mbalimbali kama vile maadili, uzazi ulio na mpango na vita dhidi ya UKIMWI, kustarehesha/ kuburudisha, kuelezea historia ya jamii, imani, itikadi na kaida za jamii pamoja na kuzipitisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine na pia huendeleza uhusiano wa kimazingira kwa kuwahusisha wanadamu na viumbe vingine vinavyopatikana katika mazingira hayo.

Nchini Kenya, vyombo vya habari, vikiwemo redio na televisheni, vimeipa fasihi hii nafasi kubwa hivyo basi kupanua hadhira yake. Nyimbo nyingi zinazosikika redioni huwahimiza watu kuwa na uwajibikaji, uzazi wa mpango, kuchagua viongozi bora na kufanya kazi kwa bidii. Lugha ya Kiswahili imetumika kuimba nyimbo zenye ushauri kuhusu mapenzi, maadili, uwajibikaji katika ndoa, n.k. Jambo hili huufanya utanzu huu kuifikia hadhira pana. Aidha, nyimbo huchukua sehemu kuu katika sherehe na mihadhara mbalimbali, iwe rasmi au isiyo rasmi, hivyo kuifanya fasihi hii kuwa muhimu sana katika jamii.

Nyimbo za Joseph Ngala ni aina mojawapo ya nyimbo zinazopendwa na watu wengi katika jamii, hasa mkoa wa pwani ya Kenya, kutokana na maudhui mbalimbali yawasilishwayo na nyimbo hizi pamoja na kuwa hutoa burudani tele kwa hadhira. Msanii huyu huwasilisha nyimbo zake katika sherehe mbalimbali. Pia huweza kupeperushwa hewani katika redio. Nyimbo hizi hufikia hadhira pana kutokana na kuwa zinatungwa kwa lugha ya Kiswahili ambapo mtunzi wazo, kupitia usanii wa hali ya juu wa lugha, huwasilisha maudhui mbalimbali. Hivyo basi, utafiti wetu ulikusudia kuchanganua baadhi ya maudhui yanayoshughulikiwa katika baadhi ya nyimbo zake, hasa tukijikita katika maudhui ya uadilifu.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Nyimbo ni sanaa ambayo inahitaji kufanyiwa utafiti zaidi kwa jinsi ambavyo watu wengi wanaweza kuzipata kupitia vyombo vya habari, hasa redio na televisheni. Sanaa hii ambayo ni moja kati ya aina za fasihi simulizi, haiwezi kupuuzwa pia kutokana na majukumu inayotekeleza katika jamii.

Utafiti wetu ulilenga kuangalia aina mojawapo ya fasihi simulizi ambayo ni nyimbo. Nyimbo tulizotafiti ni nyimbo za bango za Joseph Ngala ambazo zimetia fora sana mkoa wa pwani ya Kenya. Nyimbo hizi ni tofauti sana na nyimbo zingine zinazoimbwa pwani kwani mara nyingi huimbwa harusini, vituo vya burudani na hata siku ya kuadhimisha utamaduni wa jamii za Pwani. Nyimbo hizi huvuta sana makini ya hadhira zinapowasilishwa, jambo ambalo limetupa msukumo wa kuzitafiti.

Ngugi (2000) akimnukuu Balisidya (1987), anakubali kuwa sanaa hii ni sehemu mojawapo ya fasihi ya Kiswahili ambayo inahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi kwa jinsi ambavyo watu wengi wanaweza kuipata. Fasihi simulizi hasa ya Kiswahili, kulingana nasi haijafanyiwa uchunguzi mwingi nchini Kenya, kama ilivyo fasihi andishi, jambo ambalo limeifanya fasihi andishi ikue kwa kiwango cha juu kuliko fasihi simulizi.

Aidha, nyimbo mbalimbali zinazoimbwa mkoa wa pwani ya Kenya kama vile za taarabu, za dini, harusi, jando n.k. zimetafitiwa kwa kuchunguza masuala kama vile maudhui na mtindo katika nyimbo hizi. Nyimbo za Joseph Ngala kulingana na utafiti wetu wa awali hazijatazamwa japo zina mchango mkubwa katika kuendeleza jamii.

## 1.2 MASWALI YA UTAFITI

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i. Je, ni matendo yepi adilifu yanayojitokeza katika nyimbo tulizoteua za Joseph Ngala?
ii. Je, matendo hayo adilifu yanatoa athari zipi kwa walengwa (jamii/ mtu binafsi)?
iii. Je, kunazo sababu thabiti za kuainisha matendo hayo kama adilifu?

## 1.3 MALENGO YA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kwa ujumla kuangalia aina mojawapo ya fasihi simulizi ambayo ni nyimbo. Malengo mahsusi ya utafiti huu hata hivyo yalikuwa ni:

i. Kuchanganua maudhui ya uadilifu katika nyimbo za Joseph Ngala.
ii. Kuonyesha faida / athari za maadili katika jamii.
iii. Kuonyesha sababu thabiti za tendo kuwa adilifu.

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Fasihi ni fani iliyo hai na ambayo hutekeleza majukumu muhimu katika jamii. Fasihi simulizi, hasa nyimbo, hupewa nafasi kubwa katika maisha ya kila siku kama vile katika sherehe, redioni, shuleni n.k. hivyo ni muhimu kuifanyia utafiti zaidi ili kutoa habari zaidi kuhusu utanzu huu.

Kwa mujibu wa Wamitila (2008:10), fasihi kwa muda mrefu, tangu enzi za Aristotle na Plato, imechanganuliwa kama nyenzo ya kuendeleza maadili hivyo, fasihi ni chombo muhimu sana kinachopaswa kukitwa kwenye muktadha wa jamii ambayo inapaswa kuongozwa na kuelekezwa kimaadili. Hii inaonyesha kuwa, nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi zina jukumu kuu la kukuza maadili katika jamii, kukosoa, kupitisha utamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine, n.k.

Bukenya, A. na wengine (1994:6) wanasema kuwa, mwili/ hadhira ni kama sumaku kwa bunilizi yoyote ile; mwili ndicho kifaa ambacho bunilizi husika hutaka kunata. Sauti itokapo kinywani mwa mtendaji, huwa inaingia akilini mwa msikilizaji kupitia kwenye masikio na kumwathiri, athari ambayo huchochea matokeo kama vile kucheza, kulia, kucheka n.k. Haya yanapotokea, hatimaye lengo la ile bunilizi huweza kutimilika. Maelezo haya yanaonyesha bayana athari kuu ya fasihi simulizi kwa hadhira wakati inapowasilishwa; jambo ambalo hufanya uwasilishaji wa maudhui ya utanzu husika utimilike kwa ufanisi wa hali ya juu. Hii ina maana kuwa fasihi simulizi ina jukumu kuu la kuendeleza jamii hivyo, inahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi.

Joseph Ngala ni mtunzi ambaye huadilisha jamii kupitia nyimbo zake. Nyimbo zake pia hupewa nafasi kubwa katika sherehe na vyombo vya habari na huweza kuwafikia watu wengi kwani huimbwa kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, kadri ya ufahamu wetu, nyimbo hizi hazijapata kushughulikiwa na mtafiti yeyote. Jambo hili lilitupa msukumo wa kuchunguza maadili mbalimbali anayopitisha katika jamii kupitia nyimbo zake.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA

Utafiti wetu ulijikita katika nyimbo tisa teule za Joseph Ngala tulizochagua kama sampuli lengwa. Tulizichagua nyimbo za Joseph Ngala kutokana hali ya juu ya utunzi wake pamoja na umuhimu wake katika kuelimisha jamii.

Nyimbo tulizoteua ni: *Fuateni Mambo ya Sheria*, *Mwana Mpotevu*, *Ndivyo Ilivyo Dunia*, *Nisikilize Mwanangu*, *Ndugu Tupendane*, *Dada Vumilia*, *Simba*, *Kisulisuli* na *Jembe*. Tulizichagua nyimbo hizi kimaksudi maanake zina uzito wa maudhui tunayolenga kushughulikia kwa hivyo zitatufaa sana katika utafiti wetu. Katika utafiti wetu, tulijikita katika uchanganuzi wa maudhui ya uadilifu kama yanavyojitokeza katika nyimbo tulizochagua wala si maudhui mengine.

Katika uchanganuzi wa nyimbo hizi, tuliongozwa na mihimili minne ya nadharia ya unufaishaji hasi ambayo tumeieleza katika sehemu ya msingi wa nadharia. Mihimili hii ilitusaidia katika kushughulikia malengo yetu ya utafiti.

Katika ukusanyaji wa data tulitumia diski za nyimbo hizi pamoja na zile zilizotolewa katika mtandao. Pia tulitumia mahojiano ili kupata habari kuhusu historia ya Joseph Ngala pamoja na asili ya nyimbo za bango.

## 1.6.0 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

Katika uchunguzi tuliofanya katika majarida, vitabu na tafiti zingine zilizofanywa, si mengi yaliyoandikwa kuhusu nyimbo za Joseph Ngala. Aidha, kadiri ya ufahamu wetu, hakuna kazi yoyote inayoeleza moja kwa moja kuhusu maudhui katika nyimbo hizi za Joseph Ngala kumaanisha kuwa, suala hili halijashughulikiwa na mtu yeyote.

Hata hivyo, wapo wasomi ambao wameshughulikia utanzu wa nyimbo kwa kuzingatia masuala kama vile maudhui, mtindo na nafasi ya nyimbo katika fasihi ya Kiswahili, mchango ambao utatufaa katika utafiti wetu.

### 1.6.1Yaliyoandikwa kuhusu nyimbo kwa jumla

Wamitila (2003:107) anaainisha nyimbo kama mojawapo ya kundi kuu linalopatikana katika ushairi simulizi. Anaeleza nyimbo kama tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka, zilizotungwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Anaeleza kuwa nyimbo huchukua sehemu kubwa katika miviga ya jamii mbalimbali hivyo ni muhimu sana katika jamii. Kando na hayo, anasema kuwa nyimbo huwa na mawazo mazito na hupaniwa kuonyesha uhusiano wa kijamii, mgogoro, kukejeli, kuliwaza kutuimbuiza, n.k. Takribani shughuli zote za binadamu kama vile kulima, kujenga, unyago na jando huandamana na nyimbo na uimbaji. Kila shughuli katika msingi huu hivyo basi, huwa na aina yake ya nyimbo maalum. Nyimbo pia huwasilisha hisia mbalimbali kama vile kupenda, kuchukia, kukandamizwa, n.k. kwa njia ya kuimbwa na huwa na athari kubwa. Maelezo haya aliyotoa yanaonyesha bayana umuhimu wa nyimbo katika jamii. Maelezo haya ya Wamitila ni muhimu katika utafiti wetu kwani yalitusaidia katika kueleza umuhimu wa nyimbo za Joseph Ngala katika jamii kwa kulenga maudhui ya uadilifu.

Njogu na Chimera (1999:24) wanaeleza kuwa fasihi ina jukumu la kudumisha na kukuza uhusiano baina ya mwanadamu na jamii yake kupitia mafunzo na maadili yanayojenga mshikamano wa jamii. Wanasisitiza hayo kwa kusema kuwa jamii/ mtu anayejinyima nafasi ya kuchota kwenye chemichemi ya fasihi huwa amejikosesha fursa ya kukuza hisia zake, ubongo wake na tabia yake na kujihini fursa ya kujielewa na kuyaelewa mazingira yake. Waandishi hawa hawajaeleza umuhimu hasa wa nyimbo katika kuadilisha jamii bali wamegusia ngano, riwaya na tamthilia. Hata hivyo, maelezo yao ya umuhimu wa fasihi yalitusaidia katika kueleza umuhimu wa nyimbo katika kuadilisha jamii kwani nyimbo ni utanzu mmojawapo wa fasihi simulizi.

Ngugi (2000) katika makala yake ya nafasi ya muziki uliopendwa katika fasihi ya Kiswahili anaeleza kuwa, lengo kuu la nyimbo, kama ilivyo fasihi, ni kuelimisha na hata kuburudisha jamii. Anaeleza kuwa utanzu wa nyimbo una nafasi kubwa katika fasihi ya Kiswahili kwani huwafikia watu wengi zaidi katika jamii hasa kutokana na kutumia lugha ya Kiswahili. Aidha, anaeleza kuwa vyombo vya habari nchini Kenya vimeipa fasihi hii nafasi kubwa sana hivyo basi kupanua hadhira yake. Vilevile, Ngugi anaeleza kuwa nchini Kenya, wanamuziki wa Kenya wamegawanyika katika makundi mbalimbali ambayo ni watendaji wa muziki wa bendi, kwaya, taarabu na watendaji wa muziki wa kiasili. Anasisitiza kuwa karibu kila kundi hutumia lugha ya Kiswahili linapokuwa na ujumbe maalum kwa wananchi wote nchini.

Katika kueleza muziki uliopendwa, anasema kuwa ni muziki ulioibuka katika kipindi cha majilio ya wazungu ambapo Kenya ilishuhudia nyimbo nyingi za kutoka nje na ambazo zilianza kuonewa fahari. Hii ni kwa sababu wazungu walipofika, walimdhalilisha Mwafrika na kumteka kimawazo asiweze kuonea fahari nyimbo zake. Hili lilifanya nyimbo zilizopendelewa kuwa ni zile zilizoimbwa kwa lugha ya Kiingereza. Nyimbo hizi hata hivyo zilisikilizwa tu na watu wachache walioifahamu lugha ya Kiingereza. Waimbaji kadhaa waliendelea kutumia lugha ya Kiswahili katika nyimbo zao mathalani Fadhili William, Daudi Kabaka, John Mwale n.k. Hawa ndio walifanikisha lugha ya Kiswahili katika miaka ya sitini.

Baadaye, watu walianza kubadili msimamo wao wa kupendelea nyimbo zilizoimbwa kwa lugha ya Kiingereza na kuanza kuenzi zile zilizoimbwa kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu watu wengi waliweza kuzielewa nyimbo hizi kwa kuwa ziliitungwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hili lilifanya nyimbo za waimbaji hawa kujulikana kama nyimbo zilizopendwa hadi

sasa. Ngugi (2000) anaeleza kuwa nyimbo zilizopendwa zitaendelea kukua kufuatana na mabadiliko ya kihistoria na kifani hivyo basi, nyimbo hizi hazina budi kuchukuliwa kama sehemu moja ya fasihi ya Kiswahili kwa kuangalia mchango wake wa kimaudhui na kifani.

Maelezo haya yanaipa kazi yetu mashiko kwa sababu tunaonyesha mchango wa nyimbo za Joseph Ngala kimaudhui kwa kujikita katika maudhui ya uadilifu. Nyimbo za Joseph Ngala, kulingana na maelezo ya Ngugi ziko katika kitengo alichoeleza, ingawa kwa ujumla, cha nyimbo zilizopendwa kwani alianza kuziimba katika miaka ya hamsini. Hii ina maana kuwa zina nafasi kubwa katika fasihi ya Kiswahili kwani zina mchango mkubwa wa kimaudhui na pia wa kifani. Hata hivyo, tulijikita katika mchango wake wa kimaudhui.

### 1.6.2 Yaliyoandikwa kuhusu aina maalum za nyimbo

Owino (2011) amefanya uchunguzi wa nyimbo za kidini za Foustin Munishi kama nyimbo zenye umaarufu kimaudhui. Ameonyesha namna mwimbaji huyu anapitisha ujumbe wake kwa uzito lakini kwa kutumia mkakati wa upole. Nyimbo mbili alizochunguza hata hivyo zinagusia masuala ya uadilifu, suala ambalo hurejelewa na waimbaji wengi wa nyimbo za dini. Wimbo wa kwanza aliochanganua wa “Maji yana mdudu” unaeleza ukosefu wa maadili katika jamii unaosababisha uenezaji wa ugonjwa wa UKIMWI. Katika wimbo huu, anawahimiza waliooa kuwa waaminifu kwa wapenzi wao. Haya yako katika mshororo unaosema kuwa “Unywe maji yako peke yako na usiyashiriki nao wengine ni hatari kubwa eeh!” Vilevile, wimbo wa pili aliochambua wa “Malebo” unakashifu utumiaji wa dawa za kulevya. Anafanya hivyo kwa kumrejelea rafikiye Malebo ambaye anamsihi aokoke lakini anakataa na amepotelea katika matumizi ya dawa za kulevya ambazo zimedhuru maisha yake. Owino (2011) anaeleza namna mtunzi wa nyimbo hizi anavyopitisha maadili haya katika jamii kwa kutumia mkakati wa upole. Hata hivyo, yeye amejikita katika nyimbo za dini za Foustin Munishi, tofauti na utafiti tuliofanya ambao tulijikita katika nyimbo za Joseph Ngala.

Timammy (2002) ameeleza kwa kina namna mitindo mbalimbali inavyotumika kuwasilisha maudhui katika nyimbo za harusi za wanawake Waswahili. Ameeleza kuwa nyimbo ni usemi wenye mahadhi ulio na ubeti mmoja au zaidi na ulio na maana iliyokamilika kimuktadha. Aidha, anaeleza kuwa nyimbo ni ushairi unaotungwa ili kuimbwa katika shughuli rasmi na zisizo rasmi. Uchunguzi aliofanya unachangia kuonyesha umuhimu wa nyimbo za harusi katika sherehe za

harusi. Nyimbo alizochunguza hata hivyo zinagusia masuala ya uadilifu. Kwa mfano, kukashifu umbea, kudhibiti hasira ili kuepukana na hasara, uvumilivu, kuwajibika kwa wanaume katika ndoa n.k. Kazi hii ilitusaidia kutupa mwelekeo katika utafiti tuliofanya wa kuchunguza maudhui ya uadilifu katika nyimbo za Joseph Ngala. Hata hivyo, tofauti na tahakiki yake, hatukujishughulisha na suala la lugha.

Kasau (2013) katika tasnifu yake ameshughulikia maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo za injili za Rose Muhando. Amechanganua mafunzo muhimu yanayojitokeza katika nyimbo za Rose Muhando hivyo kuonyesha umuhimu wa nyimbo hizi za dini katika jamii. Masuala mengi yaliyoelezwa katika nyimbo hizi ni ya uadilifu. Kwa mfano, ameangazia upotofu wa maadili katika jamii kama vile mauaji, ukahaba, ponografia mtandaoni na uhusiano wa kimapenzi wa jinsia moja unaotokana na watu kuziacha njia za Mungu. Hata hivyo, nyimbo hizi zinaeleza kuwa mtu anapopotoka kimaadili lakini hatimaye kutubu/ kuomba msamaha, bila shaka Mungu atamsamehe. Tunapata kuwa hapa, nyimbo hizi zinafunza watu maadili ya kuomba msamaha wanapokosea wengine au hata wanapomkosea Mungu. Masuala mengine yanayoelezwa katika nyimbo hizi ni kama vile uchawi na ushirikina, umbea, upendo, heshima na uaminifu katika ndoa, uvumilivu katika maisha na uwajibikaji kwa kufanya kazi zinazokubalika katika jamii ili kujikimu kimaisha. Aidha, Kasau ameonyesha mbinu mbalimbali za lugha zinazotumika katika nyimbo hizi katika uwasilishaji wa maudhui. Uchanganuzi wake wa maudhui ya uadilifu katika baadhi ya nyimbo za Rose Muhando ulitufaa katika kuchambua maudhui ya uadilifu katika nyimbo za Joseph Ngala ingawa sisi hatukushughulikia lugha.

Mahugu (1990) katika tasnifu yake anachambua nyimbo za Agikuyu zilizoimbwa wakati wa kupigania uhuru nchini Kenya kwa sababu kulingana naye, jamii hii ndiyo ilihusika zaidi katika kupigania uhuru. Lengo lake lilikuwa kuchunguza maudhui katika nyimbo hizi ili kupata picha ya hali ya kisiasa iliyokuwa wakati huo na pia matamanio ya Wakenya wakati walikuwa wanapigania uhuru. Alifanya hivyo kwa kuangazia maudhui manne katika nyimbo mia moja za wakati huo. Maudhui haya ni pamoja na uzalendo wa Agikuyu, usaliti wa baadhi ya Wakikuyu, uzalendo wa kitaifa na uongozi. Haya kwa njia moja au nyingine yanagusia suala la uadilifu kwani, walioungana na kupigania uhuru walipaswa kuwa waadilifu ili wasije wakawasaliti wenzao. Mahugu kwa hivyo ameonyesha namna nyimbo hutumika katika kuielewa jamii, kama tunavyofahamu kuwa fasihi ni kioo cha jamii, jambo ambalo ni mojawapo ya majukumu ya

fasihi. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na tuliyofanya kwani tuliangazia jukumu la nyimbo kama kifaa cha kuadilisha jamii kwa kujikita katika nyimbo za Joseph Ngala.

Kieli (1988) anachanganua nyimbo za Myali za jamii ya Akamba kwa kuangazia maudhui na mtindo katika nyimbo hizi. Anaeleza kuwa, nyimbo hizi zilitumiwa kuikosoa jamii na zilikuwa maarufu sana na sehemu muhimu ya fasihi ya Akamba. Hizi ni miongoni mwa nyimbo za kitamaduni za Akamba. Wimbo mmoja kwa mfano, ungekuwa na maudhui mengi kwa hivyo alitaka kuchambua maana za ndani zilizowasilishwa na nyimbo hizi. Anasema kuwa nyimbo katika jamii hii zilikuwa na bado ni njia muhimu sana ya kujieleza. Nyimbo hizi zilikuwa muhimu sana katika sherehe tofauti tofauti za jamii husika kama vile za harusi na ile iitwayo *wathi* (sherehe ambayo wanajamii walikusanyika pamoja katika mahali paitwapo *kituto* na kuimba nyimbo hizi za Myali pamoja na zingine kama vile *mbathi sya kivalo).* Sherehe hii ilitumika kama mahali pa wanajamii kukutana na wake/ waume watarajiwa, wakati wa burudani na baada ya kazi. Alichanganua nyimbo tano kwa kuangalia maudhui na mtindo. Mchango wake wa kuchanganua maudhui katika nyimbo za *Myali* ulitupa mwongozo katika kueleza maudhui ya uadilifu katika nyimbo za Joseph Ngala.

Mjomba (2012) anaeleza suala la upole katika nyimbo saba za harusi kutoka jamii ya Wadawida kwa kutumia nadharia ya upole ya Brown Levinson (1978). Anaeleza namna lugha inavyotumika katika nyimbo za harusi za Wadawida ili kuusitiri uso wa maarusi au wa jamii. Anaeleza kuwa nyimbo za harusi za Wadawida hutungwa kwa lengo la kupitisha ujumbe wa kuwatayarisha maarusi katika majukumu tofauti tofauti ya ndoa, kuwatia moyo na hata kuwakejeli na kuwasuta waliokuwa wakiwatakia mabaya. Bibi harusi kwa mfano hufunzwa maadili anayofaa kuzingatia katika ndoa kama vile kumtii mumewe, kuwa mwaminifu, kumpikia mumewe na kukidhi mahitaji yake yote. Anaeleza kuwa wasanii wa nyimbo hizi hupitisha ujumbe huu kwa kutumia mafumbo na misemo ili kupunguza tishio la kudhuru uso hasi wa maarusi. Uchambuzi wa Mjomba (2012) wa baadhi ya maadili yanayojitokeza katika nyimbo za harusi za Wadawida, ingawa si moja kwa moja, yalitupa mwongozo katika kueleza maudhui ya uadilifu katika nyimbo tulizoshughulikia za Jospeh Ngala.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA

Utafiti wetu ulijikita katika nadharia ya uadilifu iitwayo unufaishaji hasi. Hii ni aina ya nadharia iliyo katika kundi la nadharia ambazo hupimia uadilifu kwa kutumia kigezo cha matokeo ya tendo. Hizi nadharia hueleza kuwa matokeo ya tendo maalum ndiyo huwa nyenzo thabiti ya kupima uadilifu wa tendo hilo. Kulingana na nadharia hii, tendo lolote adilifu ni lile ambalo linapunguza uchungu kwa watu wengi na lile lisilo adilifu ni lile huongeza uchungu kwa watu wengi. Maswali kama vile je, napaswa kutenda tendo lipi au je, nafaa kuwa mtu wa aina gani hujibiwa kutegemea athari ya swala husika kwa hali njema ya watu husika.

Mwasisi wa nadharia hii ni Popper (1945). Popper alikuwa mwanafilosofia wa sayansi na siasa. Nadharia hii ya unufaishaji hasi ilitokana na nadharia za awali za unufaishaji hasa ile ya Bentham (1748–1832) na Mill (1806–1873). Kulingana na watangulizi hawa, tendo adilifu ni lile liletalo athari chanya zaidi kama vile furaha na linatoa athari hizo chanya kwa watu wengi ila si kwa mtu mmoja tu. Wanaeleza kuwa kigezo cha kupima tendo adilifu au lisilo adilifu ni kile kisababishacho furaha kuu zaidi na kwa watu wengi. Walieleza haya katika kanuni ya faida isemayo kuwa tendo adilifu ni lile liletalo furaha kuu zaidi. Walieleza furaha kama kufikia upeo wa raha na kupunguza kabisa uchungu/ maumivu. Hivyo basi, tendo ambalo lina manufaa au linaloleta furaha linapaswa kutekelezwa/ kutendwa. Tofauti ya Bentham na Mill ni kuwa Bentham alijikita katika kiwango cha furaha, naye Mill alijikita katika ustahilifu wa furaha.

Kwa mujibu wa Sinha (1978), Popper (1945) aliibuka na nadharia ya unufaishaji hasi ambapo alisisitiza kuwa tendo adilifu ni lile lipunguzalo uchungu badala ya kusisitiza kuongeza furaha kama walivyofanya watangulizi wake. Hii ni kwa sababu kulingana na Popper (1945), uchungu huwa na athari kubwa zaidi kwa mpokezi wa tendo kuliko ilivyo furaha, kwa hivyo kigezo hiki ndicho kinapaswa kusisitizwa zaidi katika kuamua ni tendo lipi adilifu. Vilevile alisema kuwa katika maisha ya kila siku, binadamu huombwa hasa kusaidia binadamu anayeteseka ili kumpunguzia uchungu anaohisi au shida aliyonayo wala hakuna yule anayeombwa kuongeza furaha kwa aliye na furaha tayari. Popper (1945) pia alipinga waliyosema watangulizi wake kuwa kuongezwa kwa furaha na kupunguzwa kwa uchungu ni vitu vilivyosawa au vinavyotoa athari iliyo sawa. Kwake yeye, kupunguzwa kwa uchungu kuna athari kubwa zaidi kuliko kuongezwa kwa furaha.

Kulingana na Popper (1945) baadhi ya vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa katika kupima kiwango cha uchungu unachopunguzwa/ kuongezwa na tendo ni kama vifuatavyo:

- Ukali - uchungu utapunguzwa/ kuongezwa kwa kiwango kipi cha nguvu.
- Muda - tendo litasababisha kupunguzwa/ kuongezwa kwa uchungu kwa urefu/ufupi wa kipindi kipi.
- Uwezekano - uwezekano kuwa tendo litapunguza/ kuongeza uchungu.
- Kiwango - watu wangapi wataathiriwa na kupunguzwa/ kuongezwa kwa uchungu.

Kulingana na Popper (1945), baadhi ya mihimili ya nadharia ya unufaishaji hasi ni kama ifuatavyo:

1. Kulingana na maumbile ya binadamu, huwa anatawaliwa na mambo mawili makuu ambayo ni uchungu na furaha. Mambo haya mawili ndiyo huamua kitendo ambacho binadamu atafanya hasa kulingana na athari ya kitendo hicho. Hata hivyo, binadamu anapaswa kutenda kile ambacho kitapunguza uchungu.
2. Wahusika wanaopaswa kuzingatiwa kama wapokezi wa athari ya tendo lolote lile wanaweza kuwa jamii au mtu binafsi. Ni muhimu kuzingatia kuwa jamii huundwa kwa mkusanyiko wa watu wengi hivyo, ukitosheleza mahitaji ya mtu binafsi basi utakuwa hatimaye umezingatia jamii kwa jumla. Iwapo ni jamii inazingatiwa basi, kitendo kinachokubalika ni kile kipunguzacho uchungu kwa watu wengi katika jamii hiyo.
3. Kitendo kinaweza kubalika kama adilifu iwapo kitapunguza uchungu zaidi na kwa watu wengi.

Nadharia hii ya unufaishaji hasi ilitufaa sana katika utafiti wetu kwani ilitusaidia:

- Kuchanganua ni matendo yepi adilifu kulingana na msanii wa nyimbo hizi na ni matendo yepi anayoshauri watu kuwa nayo.
- Kuchanganua ni vipi tendo husika ni adilifu au sio adilifu hasa kwa kuangalia iwapo linapunguza uchungu kwa watu wengi.
- Kuonyesha iwapo tendo husika lina athari chanya au hasi kwa mtu binafsi au kwa jamii.

- Kuonyesha iwapo utendaji wa tendo husika umetawaliwa na kigezo cha uchungu au furaha.
- Tendo husika linaathiri mtu binafsi au watu wengi/ jamii.

Baada ya Popper (1945), kuna waandishi wengine walioendeleza nadharia hii ya unufaishaji ambao ni kama vile Adams (1976). Adams (1976) alieleza mtazamo mwingine wa nadharia ya unufaishaji ambapo alijikita katika kueleza ni sababu gani zinazomfanya mtu kutenda kitendo maalum. Hii ni kwa sababu kitendo unachotenda kinaweza kikasababisha athari mbaya lakini nia hasa ya mtenda iwe nzuri. Alieleza kuwa tunachopaswa kutumia kupimia uadilifu si athari ya kitendo bali ni nia ya mtendaji katika kutenda kile kitendo. Tatizo la mtazamo huu ni kuwa, mtu anaweza kuwa na nia nzuri ya kutenda kitendo fulani lakini kile kitendo kilete athari mbaya kwa mtendewa. Katika hali hii, tutasema kuwa kile kitendo ni adilifu?

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya unufaishaji hasi kwa mujibu wa Popper (1945). Hii ni kwa sababu mihimili yake pamoja na mtazamo wake kuhusiana na uadilifu wa tendo ndiyo ulitufaa zaidi katika kuangazia malengo yetu ya utafiti.

## 1.8.0 MBINU ZA UTAFITI

Katika mbinu za utafiti, tunafafanua mahala pa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

### 1.8.1 Mahala pa utafiti

Utafiti wetu ulijikita kwa kiasi fulani maktabani ili kupata maandishi yanayohusiana na mada tuliyoshughulikia. Vitabu na makala za mtandao zinazotoa maelezo kuhusu fasihi simulizi hasa utanzu wa nyimbo yalisomwa ili kutupa mwanga zaidi kuhusu utanzu wa nyimbo ambao tunatafiti. Yalitupa pia ufafanuzi kuhusu mihimili ya nadharia tuliyotumia katika utafiti wetu na namna tulipaswa kuitumia.Tuliangalia pia tasnifu mbalimbali zinazohusiana na nyimbo ili kupata yale yamefanywa na wasomi wengine. Haya yalitupa mwongozo katika ufafanuzi wa mada tuliyoshughulikia.

### 1.8.2 Uteuzi wa sampuli

Sampuli tuliyotumia ni sampuli lengwa ambayo ni nyimbo tisa za Joseph Ngala. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999:50), aina hii ya sampuli hutumika katika utafiti unaokusudia kupata habari za kina na bila kujumlisha. Kwa kurejelea haya maelezo, tulichagua nyimbo tisa kimaksudi maanake zilitusaidia kupata habari za kina za suala tunalochunguza la uadilifu katika nyimbo za Joseph Ngala pasipo na kujumlisha. Hii ni kwa sababu nyimbo hizi zina uzito wa maudhui tuliyoshughulikia.

### 1.8.3 Ukusanyaji data

Diski za nyimbo tisa tulizoteua katika utafiti huu zilisikilizwa na kunakiliwa. Pia, kuna zile zilizotolewa katika mtandao ambazo zilisikilizwa na kunakiliwa. Nyimbo hizi zilichunguzwa ili kubaini maudhui ya uadilifu yaliyo katika nyimbo hizi. Pia tulitumia mbinu ya mahojiano ili kupata habari zaidi kuhusu asili ya mtindo wa nyimbo za bango pamoja na historia ya Joseph Ngala.

### 1.8.4 Uchanganuzi wa data

Data tuliyoipata tuliichanganua kulingana na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia ya unufaishaji hasi. Kwa kutumia msingi wa nadharia hii, tulichanganua matendo adilifu yaliyojitokeza katika nyimbo hizi. Kwa kutumia nadharia hii, tulieleza ni sababu gani thabiti tunazotoa ili kuainisha matendo husika kama adilifu. Pia tulieleza kwa mujibu wa nadharia hii ni vigezo vipi vinavyosababisha kuwepo kwa tendo husika. Kwa mfano, ni kigezo cha furaha au uchungu. Aidha, tulieleza iwapo tendo husika linaongeza au kupunguza uchungu kwa mtu binafsi au kwa jamii. Hii ni kwa sababu hiki ni kigezo kimojawapo cha kuainisha tendo adilifu kwa mujibu wa nadharia ya unufaishaji hasi.

### 1.8.5 Uwasilishaji wa data

Baada ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo ulifanywa kwa njia ya maelezo. Uwasilishaji huu ulihusu maelezo ya maudhui ya uadilifu kwa kurejelea nyimbo tisa tulizoteua.

## 1.11 HITIMISHO

Kwa muhtasari, utafiti wetu ulilenga kushughulikia maudhui ya uadilifu katika nyimbo tisa tulizoteua za Joseph Ngala kwa kutumia mihimili ya nadharia ya unufaishaji hasi.

Katika sura hii, tumeeleza masuala muhimu yaliyoongoza utafiti wetu ambayo ni kama vile usuli wa mada, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada tuliyoshughulikia, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada tuliyoshughulikia, msingi wa nadharia na hatimaye, mbinu tulizotumia za utafiti.

Tunatarajia kuwa kwa kueleza mada hii, tutakuwa moja kwa moja tumeonyesha umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii kwa kulenga suala la uadilishaji kwani nyimbo ni aina mojawapo ya fasihi simulizi.

# SURA YA PILI

## HISTORIA FUPI YA JOSEPH NGALA NA MTINDO WA NYIMBO ZA BANGO

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sura ya kwanza, tulieleza mambo ambayo ni ya kimsingi na tuliyoyalenga katika utafiti wetu. Katika sura hii, tumeeleza historia fupi ya msanii tunayeshughulikia nyimbo zake ambaye ni Joseph Ngala, usuli wa mtindo wa nyimbo hizi na maelezo ya dhana ya maadili ambayo tunachunguza kama suala kuu linalojitokeza katika nyimbo tisa tulizoteua. Maelezo haya ni muhimu sana katika sura hii kwani yanatoa ufafanuzi kuhusu mada tunayoishughulikia ili iweze kueleweka kwa ukamilifu.

## 2.1 HISTORIA YA JOSEPH NGALA.

Joseph Ngala ni mwimbaji anayesifika wa nyimbo za bango, mzaliwa wa eneo la mji wa Frere, Kisauni- Mombasa. Joseph Ngala ana mke mmoja anayeitwa Margaret Ngala aliyemuoa mwaka wa 1962. Kulingana na mahojiano ya shirika la utangazaji la K24 (2013), alianza kuimba mnamo mwaka wa 1954 katika bendi yake ya kwanza iliyojulikana kama *Blue Boys Orchestra*. Baadaye katika miaka ya 60 na 70, aliimba katika bendi zingine ambazo ni *Bahari Boys na Teusi five*. Bendi hizi hazikuwa zake binafsi bali alikuwa ameungana na wenzake kuziunda.

Mwaka wa 1987 aliamua kuunda bendi yake, *Bango sounds* ambayo anaiongoza hadi sasa. Bendi hii ina wanabendi kumi. Hapo awali yeye ndiye alikuwa mtunzi mkuu wa bendi hii lakini sasa amewaachia wanabendi wenzake jukumu hilo la utunzi kutokana na umri wake. Kulingana na Moses Jana ambaye alikuwa awali mwanabendi wa *Bango Sounds,* wengi wa watoto wake wana talanta ya uimbaji. Wao pia huimba nyimbo hizi za bango. Mtoto wake anayeitwa Jimmy Ngala kwa mfano ana bendi yake iitwayo *Asili Band* naye Kilonga Ngala ana bendi yake iitwayo *Bango Academia*. Hawa wawili walianza kuimba katika bendi ya *Bando Sounds* lakini baada ya kukua kimuziki, wakaamua kuanzisha bendi zao. Joseph Ngala kufikia sasa ametoa albamu nne ambapo hivi sasa anashughulikia albamu ya tano.

Bendi hii hualikwa kutumbuiza watu katika maeneo tofauti ya burudani kama vile klabu ya *Jamboree* Mombasa na *Carnivore* , Nairobi hasa siku ya kuadhimisha tamaduni za jamii za pwani. Nyimbo hizi pia huchezwa sana katika stesheni za redio hasa zinazosikizwa maeneo ya pwani kama vile Pwani fm, Bahari fm, Baraka fm, na Kenya fm. Stesheni hizi huwa na vipindi maalamu ambavyo hucheza muziki wa bango pekee. Nyimbo za Joseph Ngala pia hutoa mafunzo na burudani tele kwa hadhira katika sherehe za harusi. Yeye ndiye mwasisi wa nyimbo hizi za bango nchini Kenya.

## 2.2 ASILI YA MTINDO WA NYIMBO ZA BANGO.

Kulingana na Moses Jana, bango ni aina ya muziki uliobuniwa na kufanywa uwe maarufu katika mwambao wa Afrika Mashariki hasa maeneo ya Pwani ya Kenya na Joseph Ngala. Aliubuni mtindo huu kutokana na nyimbo za zamani zilizoimbwa kwa mtindo wa rumba za waimbaji maarufu kama vile Fundi Konde, Paul Mwachupa na Baluka. Alichukua mahadhi haya kisha akaongeza mahadhi mengine kama vile ya mtindo wa *brass* na *salsa*. Waimbaji wa bango ambao wametokea hivi sasa wameanza kutumia mahadhi ya taarabu katika uimbaji wa muziki wa bango.

Kulingana na mahojiano ya shirika la utangazaji la K24 (2013), asili ya neno hili Bango ni wimbo wake uliopo miongoni mwa nyimbo zake za kwanza ujulikanao kama Pepeta Bango. Wakati mmoja alipoucheza, hadhira yake haikutaka acheze wimbo mwingine bali wimbo huo tu, ambao aliucheza hadi asubuhi. Hapa ndipo mmoja wa hadhira yake alimjia na kumwambia asitafute jina lingine la bendi yake, wajiite tu wanabango. Toka hapo ndipo bendi yake ikaitwa *Bango sounds*, nao mtindo wa nyimbo zake ukaitwa Bango. Nyimbo hizi mara nyingi huwasilishwa moja kwa moja kwa hadhira. Chombo kikuu atumiacho katika uimbaji wake ni saksofoni ingawa mwanzoni alianza kwa kutumia zumari. Vyombo vingine ni kama vile piano, gita, tarumbeta na ngoma.Vipo vikundi vingine ambavyo vimeibuka na kuiga mtindo wake Joseph Ngala wa uimbaji ambavyo ni kama vile Them Mushroom, Utamaduni cha Jimmy Ngala, Asenas cha Moses Jana na Tutu Jaz Band cha Juma Tutu.

## 2.3 DHANA YA MAADILI

Kila wakati maishani mwetu tunapokaa na kufikiria kuhusu matendo ya binadamu, yawe yetu au ya wengine, huwa tunajiuliza kuhusu wema wake au ubaya wake. Tunaweza tukatambua njia bora/ adilifu ya kutenda au njia mbaya/ isiyo adilifu ya kutenda. Pia, tunaweza tukarejelea mtu kama rafiki mzuri au mbaya au mtu afanyaye kazi vizuri au vibaya. Hii inaonyesha kuwa kila mara huwa tunatathmini ulimwengu halisi ambapo ni kwa kutumia maamuzi ya uadilifu ndipo tunaweza kulinganisha yale yanayotendeka na yale tunayofikiria yanapaswa kutendeka. Haya hutusaidia kufahamu iwapo tunayotathmini ni adilifu au si adilifu. Hii inaonyesha kuwa suala la uadilifu linahusiana sana na takribani shughuli zote za binadamu. Tunaweza tukasema kuwa mtu hubainishwa na matendo yake; iwapo matendo yake ni mabaya/ si adilifu basi yeye ni mbaya/ si mwadilifu na iwapo matendo yake ni mazuri/ adilifu basi, yeye ni mzuri/ mwadilifu. Hii ndio sababu maadili ni muhimu sana katika ulimwengu halisi kwani, kila mtu hutaka kuwa mzuri kwa watu hivyo, tunahitaji kujua tunapaswa kutenda vipi ili tuwe wazuri kwa watu.

Ni muhimu hivyo basi kueleza maadili ni nini. Wataalamu wengi wanakubali kuwa dhana hii ni pana sana na changamano kuieleza hasa kutokana na kukua kwa viwango vya teknolojia katika jamii ambavyo vimefanya maamuzi ya uadilifu yawe magumu kuyafanya. Hata hivyo kuna baadhi ya maelezo ambayo yametolewa kuhusu dhana hii. Mojawapo ya maelezo haya ni kuwa:

> Maadili ni dhana ambayo huhusika na masuala kama vile ni yepi yafaayo na yepi yasiyofaa, kuweza kutofautisha masuala hayo mawili na hatimaye, kuweza kuthibitisha tofauti yake. (Rae: 1973:10) (Tafsiri yangu)

Maelezo haya yanaeleza mojawapo ya masuala muhimu ya dhana ya maadili kwani unapozungumzia maadili, unapaswa kuonyesha ni yepi yanayofaa na yepi hayafai kisha utoe sababu thabiti za kutoa madai haya huku ukionyesha tofauti iliyopo kati ya mambo hayo mawili. Hata hivyo, hakueleza kuwa maadili hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kutokana na tofauti kama vile za kidini, utamaduni na pia sheria zinazotawala jamii husika.

Dhana hii pia hutumiwa kurejelea viwango vilivyo na msingi bora vya kuamua ni tendo lipi linalofaa (adilifu) na lipi lisilofaa (si adilifu); viwango vinavyoamua ni tendo lipi binadamu atende na lipi asitende kwa misingi kama vile haki, wajibu, manufaa kwa jamii n.k. Vipimo hivi

hueleza sababu zilizo na msingi za kukataza matendo kama vile kunajisi, kuiba, kudhulumu, ulaghai n.k. Viwango hivi pia hutetea haki kama vile ya kuishi na uhuru wa faragha.

Kwa mujibu wa Thompson (1999: 5), ili kuweza kutoa sababu zilizo na msingi za iwapo tendo ni adilifu au si adilifu, inafaa kuzua mjadala wa kimaadili ulio na elementi tatu bainishi ambazo ni ukweli, kaida na mantiki katika mjadala husika. Katika elementi hizi yafuatayo ndiyo yanayopaswa kuzingatiwa:

i. Ni muhimu sana kufahamu ukweli kuhusu hali husika kwa kuzingatia yafuatayo:
   - Sheria zinasema nini kuhusu hali hiyo?
   - Iwapo anayehusika katika hali hiyo ni mfuasi wa dini fulani, dini hiyo inasema nini kuhusu hali kama ile?
   - Unapaswa kuelewa vyema hali husika yaani, nia ya mtendaji ilikuwa nini na matokeo yaliyotarajiwa yalikuwa yepi.
   - Unapasa pia kujua kama kuna hali maalum hasa inayofanya hali inayochunguzwa kuwa ya kipekee kwa sababu kila hali huwa ya kipekee maanake hakuna watu wawili walio sawa.

ii. Unapaswa kuzingatia kwa makini kaida na desturi ambazo zinahusika katika kutathmini hali ile. Unapoeleza kuwa tendo fulani ni adilifu au si adilifu, unapaswa kufahamu msingi unaotumia kueleza hivyo na kaida zinazojitokeza kupitia kwa tendo hilo.

iii. Aidha, unapaswa kuzingatia mantiki katika mjadala unaozua yaani, madai yako ni yepi na changamoto unazoweza kukumbana nazo kuhusu madai hayo.
   Hii ni kwa sababu mtu anaweza akapinga unayodai kuwa ni adilifu au si adilifu kwa kusema kuwa hayo unayodai ni mapendeleo au maoni yako tu. Ili kujitetea, unapaswa kufikiria kwa makini msingi ulio na mantiki utakaotumia.

Kwa kutumia elementi hizi tatu, inawezekana kuzua mjadala katika kutathmini iwapo tendo ni adilifu au si adilifu na hatimaye kuweza kuibuka na uamuzi mwafaka.

Linalojitokeza katika maelezo ya maadili ni kuwa, maadili huhusika na matendo yanayokubalika, ukubalifu ulio na msingi thabiti. Katika utafiti wetu, tumetumia maadili kama dhana ambayo hurejelea matendo yanayofaa au yanayokubalika katika jamii maalum. Katika kueleza maadili, maswali muhimu ambayo tutajiuliza ni kama vile:

i. Mtu mwadilifu ni yupi?
ii. Maisha mazuri yanahusu nini?
iii. Jamii nzuri hukaa vipi?
iv. Ni njia ipi nzuri zaidi ambayo binadamu anafaa kuishi?

Kwa mujibu wa Ruggiero (2012), suala la maadili linaweza kuchunguzwa kupitia njia zifuatazo:

i) *Maadili fafanuzi:* Hii ni njia ambayo huchunguza maamuzi tofauti ya maadili na thamani yake katika jamii maalum. Hueleza tendo fulani bila kuchunguza iwapo ni adilifu au si adilifu.

ii) *Maadili sanifishaji*: Hueleza kanuni ambazo watu hufuata ili kufanya maamuzi ya masuala ya uadilifu. Hueleza tendo fulani na kuchunguza iwapo tendo hilo ni adilifu au si adilifu.

iii) *Maadili tumikizi*: Huchunguza maamuzi ambayo hufanywa katika nyanja mbalimbali kwa kujikita katika nadharia za uadilifu. Nyanja hizi ni kama vile maisha na kifo, matibabu, ufeministi, ujinsia, sharia, mazingira n.k.

iv) *Maadili lugha*: Huhusika na kuchunguza lugha inayotumika kueleza maadili na jinsi inavyoweza kuthibitishwa kama lugha ifaayo kufanya hivyo. Badala ya kueleza ni vipi tendo fulani ni adilifu, kitengo hiki huchunguza tunamaanisha nini tunaposema tendo fulani ni adilifu.

Katika utafiti wetu, tumeeleza maadili kwa kutumia njia ya maadili sanifishaji kwani, tumeeleza ni kanuni gani tunayotumia ili kusema tendo fulani ni adilifu. Tumefanya hivyo kwa kutumia kanuni ya faida ya nadharia ya unufaishaji ambayo inasema kuwa tendo adilifu ni lile liletalo furaha kuu zaidi na kwa watu wengi na kupunguza uchungu kwa watu hao.

Kulingana na Dobeljuh (2006), lengo la maadili ni kuweka mfululizo wa kanuni na kigezo cha kufanya maamuzi ambacho kinaweza kuwa msingi wa kufanyia marejeleo ili kutupa mwongozo wa kufanya maamuzi yetu yanayoonyesha uwajibikaji. Maadili huakisi maana ya kina ya maisha adilifu; hulenga kugundua lengo la maisha ya binadamu yeyote yule ili kuyakinisha ni matendo yepi yanayoweza kumfanya mtu kufikia lengo lake la maisha ambalo hasa ni furaha. Maadili hivyo humsaidia binadamu kuishi maisha yaliyo na utu.

Swali tunalopaswa kujiuliza kuhusu maadili ni kuwa, ni nini hasa hufanya maadili yawepo maishani au ni vigezo vipi tunavyopaswa kuzingatia ili kuweza kufahamu iwapo tendo husika lina uwezo wa kutathminiwa katika misingi ya maadili? Tumetangulia kueleza kuwa maadili huhusika na matendo ya binadamu, maamuzi wanayofanya binadamu na namna wanavyothibitisha uhalali wa maamuzi hayo. Kwa sababu hii, kuna mambo matatu yanayohitajika ili kulifanya tendo lolote lile liweze kutathminiwa katika misingi ya maadili ambayo ni:

i. Tendo la kibinadamu.

   Mashine kama vile tarakilishi ambayo haina uwezo wa kufikiria haiwezi ikalaumiwa kwa lolote itendalo maanake inapokosa kutekeleza inalopaswa, anayefaa kulaumiwa ni anayetengeneza programu katika tarakilishi ile wala si tarakilishi yenyewe. Aidha, atekelezaye mauaji kwa kutumia kisu hawezi akakilaumu kisu kwa kumdunga mhusika bali ni yeye wa kulaumiwa. Hii ina maana kuwa ili kuzua mjadala wowote wa kimaadili, lazima pawe na mtendaji ambaye ni binadamu wala si vitu visivyo na uhai.

ii. Fikra zilizo na urazini.

   Matendo yaliyo ya kimaadili/ yasiyo ya kimaadili yanafaa kuwa yametendwa na mtendaji aliye na ufahamu/ utambuzi. Hii ni kwa sababu mtendaji asiye na ufahamu hana uwezo wa kutathmini hali fulani na kuamua atende vipi. Kwa mfano, huwezi ukamhukumu mtu anayepata mshtuko wa moyo wakati anaendesha gari na kusababisha ajali inayosababisha kifo kwa mtu mwingine. Ingawa katika hali hii tendo la mauaji limetokea, huwezi ukasema kuwa mtendaji amekosa maadili kwa sababu tendo hilo lilipotendeka, mtendaji hakuwa katika ufahamu wake au alikosa urazini. Hata hivyo, ikiwa mtendaji yule alikuwa amekanywa na daktari kuendesha gari kutokana na ugonjwa wa moyo kisha akayapuuza maagizo yale na kuendesha gari, jambo linalosababisha kifo basi, tendo lile utasema kuwa si adilifu. Hii ni kwa sababu akifanya uamuzi wa kupuuza maagizo ya daktari ya kutoendesha gari alikuwa katika hali ya urazini.

iii. Uhuru.

Ikiwa mtendaji yuko huru kuchagua atakalotenda basi, anapaswa kuwa tayari kukabiliana na matokeo ya maamuzi yake. Watu wengi wanapohukumiwa kwa kutenda jambo lisilo adilifu/ lisilo halali hujitetea kuwa hawakuwa na uhuru wa kufanya uamuzi mwingine isipokuwa walioufanya. Hii ina maana kuwa tendo si adilifu iwapo mtendaji alikuwa na uhuru wa kuchagua tendo lililo kinyume na hilo. Huwezi ukamhukumu mtu kuwa amefanya tendo lisilo adilifu ilhali alilazimishwa kulitenda au hakuwa na uhuru wa kuchagua kutolitenda.

Suala la mjadala ambalo hujitokeza kuhusu maadili ni kuwa je, tunapaswa kuyahusisha na masuala kama dini, hisia na hata sheria? Iwapo tutahusisha maadili na dini, swali la kujiuliza ni je, watu ambao hawaamini kwamba kuna Mungu hawana maadili? au jamii ya watu hawa haitakuwa na maadili?. Iwapo tutayahusisha maadili na sheria, uhusiano huu utakuwa na upungufu kwani kuna baadhi ya sheria katika nchi tofauti ambazo hukosa uadilifu. Kwa mfano, sheria iliyokuwapo zamani katika nchi ya Afrika Kusini ya ubaguzi wa rangi haikudhihirisha uadilifu ndio sababu baadaye ilitupiliwa mbali. Tukihusisha maadili na hisia pia tutapotoka kwani wakati mwingi hisia hupotosha kwani hukosa urazini. Kutokana na utata huu, tumechukulia kuwa njia bora ya kueleza maadili ni ile tuliyotangulia kueleza kuwa ni kwa kutumia vipimo vilivyo na msingi bora na vinavyojikita katika masuala kama vile haki na manufaa kwa jamii, vipimo vinavyoeleza sababu zilizo na msingi za kukataza matendo kama vile kunajisi, kuiba, kudhulumu, ulaghai n.k.

Kwa nini basi tusisitize suala la maadili katika jamii? Sababu kuu ya mtu kuwa mwadilifu ni kuwa ni nguzo muhimu ya mambo mengi ambayo humkamilisha binadamu. Kwa watu wengi, kuwa na tabia adilifu ni jambo muhimu sana ambalo humfanya mtu kufanikiwa maishani mwake. Kwa mfano, ni vigumu kusema kuwa mtu amefanikiwa maishani mwake ikiwa pesa ambazo zimemfanya afanikiwe amezipata kwa njia isiyo halali kama vile wizi. Pia ni vigumu kusema mtu amefanikiwa sana katika taaluma yake lakini si mwaminifu kwa mkewe/mumewe, anawadhulumu watoto wake au anatumia dawa za kulevya. Kwa upande mwingine, tutasema kuwa mtu kama Mama Teresa ni kielelezo cha wanaoishi maisha mema ingawa hakuwa na vitu vingi hasa vya anasa ambavyo watu wengi katika jamii huthamini.

Mama Teresa alikuwa mmishenari wa dini ya Katoliki aliyeishi kati ya mwaka wa 1910-1997. Yeye ndiye mwanzilishi wa shirika la dini ya Katoliki liitwalo Wamishenari Wafadhili. Lengo la hili shirika ni kufadhili hospitali za wagonjwa mahututi na makao ya walioathiriwa na virusi vya UKIMWI, kifua kikuu na ukoma. Mwaka wa 1948, aliliacha shirika lake la awali la Loreto  na kutoka kwenye jumuia yao ya watawa ili kwenda kuwahudumia walio maskini kupindukia katika jamii hasa ya India, waliokosa mavazi na chakula, waliokataliwa katika jamii, waliougua magonjwa kama ukoma na walioathiriwa na virusi vya UKIMWI. Hapa ndipo alipoanzisha shirika la Wamishenari Wafadhili. Alifungua hospitali nyingi India na nchi zingine ambazo zilihudumia wagonjwa bila malipo na pia ziliwapa hifadhi wakongwe waliokuwa maskini na waliokaribia kufa ili wafe katika hali tulivu. Hakujali maisha yake wala kujali kumiliki mali katika maisha yake bali alilenga kuwapa matumaini walioyakosa katika jamii. Hii ndiyo sababu alipewa tuzo la zawadi ya amani ya Nobel mwaka wa 1979 kisha akatangazwa kama Mbarikiwa Teresa wa Calcutta mwaka wa 2003. Maelezo haya yanaonyesha kuwa, ingawa Mama Teresa hakumiliki mali yoyote, alifadhili wasiojiweza katika jamii, kwa hivyo alifanikiwa maishani mwake kwani aliishi maisha yaliyo mema.

Ni muhimu pia kuwa mwadilifu sababu ni nguzo katika ustawi wa binadamu, maanake kutenda mema maishani na kuwa mzuri/ mwadilifu maishani ni mambo ambayo huthaminiwa sana na watu wengi. Watu wengi hawangetaka kuishi katika jamii ambayo maadili hayatiliwi maanani. Jamii yoyote pia haiwezi kuendelea iwapo haizingatii maadili muhimu kama vile haki na ukweli.

Maadili pia ni njia ya kuelekeza kuhusu maamuzi ya kutenda tendo fulani; bila yake matendo yangetendwa kiholela. Hii ni kwa sababu watu hukumbana na hali tofauti zinazohitaji uchaguzi kila uchao. Maamuzi ambayo watu hufanya kila siku huhusu swali la ni lipi lifaalo/ adilifu na lipi lisilofaa/ si adilifu. Maadili basi humpa mtu msingi wa kuweza kufanya maamuzi haya.

Utafiti ambao tulifanya ulichanganua matendo adilifu ambayo Joseph Ngala anahimiza jamii kuwa nayo katika nyimbo zake tisa ambazo tuliteua. Tumebainisha maadili haya kwa kujikita katika maelezo ya maadili ambayo tumetangulia kutoa.

## 2.4 MAELEZO YA NYIMBO

Utafiti ambao tumefanya umeeleza maudhui ya uadilifu katika nyimbo tisa za Joseph Ngala kwa hivyo ni muhimu kueleza utanzu wa nyimbo. Nyimbo ni utanzu wa ushairi unaopatikana katika fasihi simulizi. Utanzu huu huchukua nafasi kuu katika jamii. Wamitila (2003) anaeleza nyimbo kama tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka ambapo nyimbo hizi hutungwa kwa lugha ya mvuto, matumizi ya taswira na mapigo ya silabi. Utafiti ambao tumefanya unachukulia kuwa nyimbo ni zaidi ya sauti tu ambazo huimbwa na kuchezwa kwa sababu nyimbo huwasilisha maudhui mbalimbali katika jamii husika.

Nyimbo hutekeleza majukumu mengi katika jamii kama vile kuelimisha kuhusu masuala mbalimbali kama vile maadili na uzazi ulio wa mpango, hustarehesha / huburudisha, huelezea historia ya jamii, imani, itikadi na kaida za jamii pamoja na kuzipitisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kutokana na majukumu mbalimbali ambayo yanatekelezwa na nyimbo, kuna aina mbalimbali za nyimbo kama ifuatavyo:

i. Nyimbo za harusi: Hizi ni nyimbo ambazo hutumiwa kushauri wanaofunga ndoa kuhusu namna wanavyopaswa kuishi kama mume na mke. Huwapongeza pia kwa kuchukua hatua ya kufunga ndoa. Aidha, nyimbo hizi huimbwa ili kuwasifu wazazi na maarusi kwa malezi mema, kusifu utanashati wa bwana arusi na urembo wa bibi arusi. Mahasidi nao waliodhani kuwa harusi haitafaulu hukashifiwa. Mfano wa wimbo wa harusi ni ule wa *Billy na Susan* ulioimbwa na Joseph Ngala; katika ubeti wa pili na tatu anaposema kuwa:

> Shangwe zetu ni kwa ajili, yenu Billy na Susan
> Rabai na Bamburi, leo vigelegele
> Kumepambazuka vizuri, ili tumwage Susan
> Mama Biye na Kheri waone raha.
>
> Tutamtamani Susan, yuaenda zake Rabai
> Sote twawatakia heri, maisha mazuri
> Billy wamtwaa Susan, sasa ujue ni wa kanuni

Kwa raha au shida, muwe pamoja

Lile lilopangwa na Mola, halina lile wala hili

Lenu ni pendo la ukweli, Billy na Susan.

Wimbo huu unakusudia kushangilia harusi ya Billy na Susan. Unaonyesha namna wazazi wa maarusi walivyo na furaha kwa watoto wao kufunga ndoa. Kulingana na wimbo huu, ndoa hii imetokana na upendo ulio wa kweli. Wimbo huu vile vile unakusudia kuwatakia maarusi heri na fanaka maishani mwao. Bwana harusi anakumbushwa kuwa mkewe sasa ni wake wa halali na milele hivyo wawe tayari kuishi pamoja; iwe ni wakati wa raha au shida. Upendo walio nao maarusi umewapa raha ya kufunga ndoa. Wazazi wao nao pia wamefurahi kuwaoza watoto wao hivyo sifa ya upendo ni adilifu na tendo la kufunga ndoa pia ni adilifu.

ii. Bembelezi/ bembezi: Hizi ni nyimbo zitumiwazo kuwabembeleza watoto ili walale. Hususan huimbwa na walezi wa watoto kwa mahadhi ya chini ili kuwaongoa watoto walale. Huwapa watoto matumaini kuwa mama yao atafika karibuni na kuwaletea zawadi.

iii. Wawe na Kimai: Wawe ni nyimbo za wakulima ambazo huimbwa na wakulima wakati wa kazi. Huziimba ili kuwatia shime ya kuendelea kufanya kazi. Nyimbo hizi pia huonyesha hisia zao kuhusiana na kazi yao ya ukulima. Kimai nazo ni nyimbo ambazo huhusishwa na mabaharia. Nyimbo hizi huyaeleza maisha yao, uzoefu wao na mambo wanayopambana nayo katika shughuli zao za uvuvi.

iv. Mbolezi/ tahalili: Ni nyimbo ambazo huimbwa wakati wa maombolezi/ kilio hasa kutokana na kifo. Nyimbo hizi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine na pia labda umri wa aliyeaga dunia. Huonyesha mtazamo wa jamii kuhusu dhana ya kifo.

v. Nyimbo za kisiasa: Hili ni kundi pana kwani linahusisha nyimbo kama vile za kitaifa. Hata hivyo, ni nyimbo ambazo huhusu masuala ya kisiasa. Zinaweza kutumiwa kuwaleta watu pamoja kisiasa, kuwashawishi watu kisiasa ili kuegemea katika upande fulani wa kisiasa au hata kuwakashifu wanasiasa.

vi. Nyimbo za kimapenzi: Hizi ni nyimbo ambazo huimbiwa mtu na mpenziwe ili kuelezea hisia zake za kimapenzi. Huwa na matumizi ya lugha iliyojaa ufundi wa hali ya juu na hulenga kunata hisia za anayeimbiwa. Hisia ambazo hujitokeza katika nyimbo za kimapenzi zinaweza kuwa ama za furaha au za masikitiko kwa mtu aliyeachwa na mpenzi wake au kukataliwa na ampendaye. Mfano ni wimbo wa mapenzi wa msanii Joseph Ngala uitwao *Ntachonga Sanamu*. Wimbo huu unahusu msimulizi ambaye amekataliwa na mpenziwe. Unaonyesha namna alivyotamauka kwa kukataliwa na anayempenda. Anasema kuwa amechoka kumngoja kiasi cha kukata tamaa ya kumpata mpenziwe ingawa yuampenda sana. Haya ni kama inavyotokea katika ubeti wa kwanza:

> Nimekata tamaa kwako kabisa, sina matumaini ooh
> Nitachonga sanamu, yenye kufanana na wewe
> Nitaipamba kwa maua mazuri, na vito vya thamani
>
> Ili iwe ni kama ukumbusho, kwako moyoni
> Wenye kusubiri endeleeni, mimi nisameheni ooh
> Kwa kuwa moyo sasa, umeshafika ukingoni.

Wimbo huu unadhihirisha hisia za huzuni kwani msimulizi anasikitika kwa kukataliwa na anayempenda. Amemngoja sana kwa matumaini kuwa atakuja kumkubali lakini hatimaye anakata tamaa kwa hivyo anaamua kuchonga sanamu inayofanana naye ili iwe kumbusho lake kwake.

vii. Nyimbo za kazi/ hodiya: Hizi ni nyimbo ambazo kwa jumla zinahusu shughuli za kazi ambapo kuna aina nyingi za nyimbo za kazi kutegemea shughuli ya kazi husika. Hutumiwa kutia shime wanaofanya kazi.

viii. Nyimbo za watoto: Hizi ni nyimbo ambazo huimbwa na watoto wenyewe hasa wanapocheza. Husaidia watoto kuwa wabunifu maanake wakati mwingi huwa wanazitunga wenyewe.

ix. Nyiso: Hizi ni nyimbo ambazo huimbwa jandoni (kwa wavulana) na unyagoni (kwa wasichana). Nyimbo hizi hulenga kuwatia moyo wanaotahiriwa ili wawe wakakamavu hasa wanaume wanapokabiliwa na kisu cha ngariba. Pia huwajuza kuhusu majukumu mapya na matarajio ya jamii kwao.

x. Nyimbo za maadili: Hizi ni nyimbo ambazo hukusudia kuwashauri wanajamii wawe watu wa kutenda mema na wajiepushe na maovu. Huonyesha manufaa ya kuwa waadilifu katika maisha. Matendo yasiyo adilifu hukashifiwa. Mwimbaji hufanya hivyo kwa kuonyesha athari mbaya apatazo mtu kwa kutenda matendo yasiyo adilifu. Baadhi ya nyimbo kama vile za harusi, mapenzi, nyiso na dini hutumiwa kama nyimbo za maadili. Mfano wa wimbo wa maadili ni huu wa Joseph Ngala ambao unaitwa *Bado Siku Mbili*. Ubeti wa kwanza na wa tatu unasema kuwa:

Aisee ungali kijana, wakua ndivyo inavyoonekana
Una mengi huyajui, kwa hivyo chunga dunia
Bado siku mbili tatu utaniambia x4

Mapenzi huwa ya wawili, na wa tatu huwaletea udhia
Je umekuwa bendera, pande zote wapepea
Bado siku mbili tatu utaniambia x4

Mwimbaji anakusudia kuelimisha jamii kuhusu kuchukulia mambo kwa utaratibu na kwa tahadhari maanake dunia ina mazuri na mabaya. Aidha, anakusudia kufunza waliofunga ndoa kutowasikiliza watu wengine kwani watawapotosha na kuwafanya wakosane.

Joseph Ngala ni mtunzi ambaye ameandika nyimbo tofauti tofauti. Hata hivyo, nyimbo nyingi zake ambazo tumekumbana nazo ni za maadili, mapenzi na za harusi. Kama tulivyotangulia kueleza, aina za nyimbo kama vile za mapenzi na harusi ni za maadili. Hii ni kwa sababu nyimbo nyingi za harusi hulenga kufunza wanaooana kuwa waadilifu katika ndoa ili waishi maisha ya furaha na masikizano. Baadhi ya maadili ambayo huhimizwa katika ndoa ni kama vile uaminifu, ukweli na mapenzi ya dhati. Nyimbo za mapenzi nazo hueleza umuhimu wa kupendana kwa mapenzi ya dhati. Utafiti ambao tumefanya umejikita katika baadhi ya nyimbo za maadili za Joseph Ngala ambapo tumechanganua maudhui ya uadilifu anayozungumzia katika nyimbo hizo.

## 2.5 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeangazia historia fupi ya Joseph Ngala, asili ya mtindo wa nyimbo za bango, maelezo ya dhana ya uadilifu na ya nyimbo. Haya yanatoa mwanga kuhusiana na suala tunaloangazia la maudhui ya uadilifu katika nyimbo za Joseph Ngala katika sura zifuatazo. Vilevile tumeeleza nyimbo za Joseph Ngala ni za aina gani kulingana na aina tofauti za nyimbo ambazo tumeelezea.

# SURA YA TATU

## MAUDHUI YA UADILIFU KATIKA NYIMBO ZA JOSEPH NGALA

### 3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tumeshughulikia maudhui ya uadilifu ambayo yamejitokeza katika nyimbo za Joseph Ngala. Maudhui ya uadilifu tuliyochanganua yamejikita katika muktadha wa jamii ya Kenya kwa jumla maanake kama tulivyoeleza katika sura iliyotangulia, kila jamii huwa na kanuni na vipimo vya matendo yafaayo na yasiyofaa. Uchunguzi huu tumeufanya kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya unufaishaji hasi. Aidha, malengo ya utafiti yamezingatiwa katika uchanganuzi huu. Maudhui tuliyoangazia ya uadilifu ni pamoja na:

i. Kutii sheria
ii. Kutokuwa na tamaa
iii. Kusikiliza mawaidha ya wakuu/ wazazi
iv. Upendo
v. Uvumilivu
vi. Shukrani
vii. Ushirikiano
viii. Uwajibikaji

### 3.1 KUTII SHERIA

Kuna uhusiano mkubwa kati ya sheria na maadili. Kwa mujibu wa kamusi ya Kiingereza ya Collins (1979), sheria ni kanuni zinazotungwa na bunge la nchi fulani ili kusimamia taratibu za nchi hiyo na ambazo ni lazima zifuatwe na watu waliomo humo na anayekwenda kinyume nazo hupewa adhabu na mahakama. Maadili nayo hueleza yanayokubalika katika jamii. Hueleza namna watu wanapaswa kuingiliana katika jamii katika hali itakayofaidi kila mtu. Sheria kwa hivyo hutumika ili kuhakikisha kuwa yanayokubalika katika jamii/ yaliyoadilifu yamefuatwa na anayeenda kinyume nayo amehukumiwa. Nadharia ya unufaishaji tunayotumia inaeleza kuwa sheria hizi zinapaswa kutumia kigezo cha furaha na uchungu pekee katika kuamua iwapo tendo ni adilifu au si adilifu. Hata hivyo, ni muhimu kugundua kuwa kuna wakati ambapo yanayochukuliwa kuwa ni adilifu huwa ni halali kwa mujibu wa sheria husika au pia kuna

wakati ambapo yanayochukuliwa kuwa si halali huwa ni adilifu kwa mujibu wa sheria husika. Aidha, matendo fulani yanaweza kuchukuliwa kuwa ni adilifu na kundi fulani la watu lakini kundi lingine lichukulie kuwa si adilifu. Katika hali hii, sheria ni muhimu ili kuweza kusawazisha mitazamo ya watu kuhusu matendo kama haya ili kuondoa ukinzani kuhusu uadilifu wa matendo husika.

Utapata mara nyingi kuwa sheria hujikita katika maadili ya jamii husika. Hata hivyo, hatuwezi tukasema kwa uhakika kuwa sheria ni nguzo ya maadili au sheria kila wakati husisitiza matendo adilifu. Viwango vya maadili hushirikishwa katika sheria wakati wanajamii wengi huwa na maoni kuwa viwango hivi vya maadili vinapaswa kuhalalishwa kupitia sheria. Sheria wakati mwingine hutupiliwa mbali wakati ambapo zinakiuka maadili katika jamii kama ilivyotokea Afrika Kusini kuhusiana na sheria ya ubaguzi wa rangi. Hili ni thibitisho kuwa maadili huathiri sana sheria. Theodores na wengine (2002:158) wakimnukuu Bentham (1978) wanasema kuwa, sheria za nchi zinapaswa kuhusishwa na wema halisi wa jamii husika. Wema unaorejelewa hapa ni furaha kuu kwa jamii husika. Yaliyo katika sheria ndiyo huchukuliwa na jamii kuwa adilifu na kulingana na nadharia ya unufaishaji yanapaswa kuwa ni yale yataleta furaha kuu kwa wanajamii wengi. Pia wanasema kuwa, avunjaye sheria kwa kutenda tendo linalosababisha uchungu kwa wanajamii wengi basi, anapaswa kupewa adhabu ili jamii ilindwe isidhuriwe na mtu huyu au adhabu itakayolenga kumbadilisha.

Joseph Ngala anaeleza kuhusu maadili ya kufuata sheria katika wimbo wake ambao ni *Tufuateni Mambo ya Sheria.* Kufuata yaliyo katika sheria kama tulivyotangulia kueleza huchangia katika kuleta amani na utangamano katika jamii. Kuvunjwa kwa sheria hizi kuna athari ambayo ni adhabu ya kifungo kama inavyoelezwa katika ubeti wa kwanza ambapo msimulizi anasema kuwa:

> Jama fuateni mambo ya sheria
> Usipofuata utapata taabu sana
> Kama fulani anunua mali ya wizi
> Baada ya saa namkuta kifungoni.

Joseph Ngala anaeleza maadili ya kufuata sheria kupitia usimulizi wa kijana fulani ambaye alinunua mali ya wizi ili kuiuza kisha akashikwa na kutiwa gerezani kwa miaka saba na kazi

ngumu. Anamsikitikia maanake ni kijana mdogo aliyetaka kupata faida kubwa kwa haraka kwa vile mara nyingi bidhaa za wizi huwa ni za bei ya chini.

Tendo hili la kufuata sheria linaweza kutathminiwa kwa msingi wa maadili kwa sababu limetosheleza mahitaji aliyoeleza Dolbeljuh (2006) ya kuliwezesha tendo kutathminiwa katika msingi wa maadili. Hii ni kwa sababu kwanza, ni tendo la kibinadamu wala si la kifaa kisicho na uhai kama vile mashine. Mtendaji wa tendo la kutii sheria katika wimbo huu ni kijana ambaye anatarajiwa kuwa na ufahamu wa ni lipi lifaalo na ni lipi lisilofaa. Pili, kwa kurejelea kigezo cha fikra zilizo na urazini, kijana anayezungumziwa alifanya uamuzi wa kuuza mali ya wizi akiwa katika hali ya urazini. Alikuwa na ufahamu kamili wa kumwezesha kufanya uamuzi mwafaka wa kutonunua mali ya wizi. Tatu, kwa kurejelea kigezo cha uhuru, mtendaji ambaye ni kijana alikuwa na hiari ya kuchagua anunue mali ya wizi au asiinunue maanake imebainika katika wimbo huu kuwa hakulazimishwa kununua mali ya wizi. Iwapo alilazimishwa, hatungepaswa kulitathmini tendo hili kama adilifu au si adilifu. Maelezo ya vigezo hivi yana maana kuwa tunaweza kulitathmini tendo la kufuata sheria kwa misingi ya maadili, yaani iwapo ni adilifu au si adilifu maanake limetosheleza mahitaji tuliyoeleza.

Tendo hili la mhusika linamsababishia uchungu kutokana na kufungwa gerezani kwa miaka saba na kupewa kazi ngumu. Uchungu huu unaompata mhusika unatokana na hukumu ya adhabu inayotolewa na jaji mahakamani kwa mujibu wa sheria husika. Adhabu hii ya kifungo cha miaka saba gerezani na kazi ngumu inaongeza uchungu kwa kijana mhusika. Hii ni kwa sababu kijana mhusika anahisi uchungu kwa kutokuwa na pesa ndiposa anauza mali ya wizi ili aweze kupata pesa atajirike kwa haraka hivyo apate furaha. Hata hivyo anafungwa gerezani kwa hivyo tendo lake la kuuza mali ya wizi linamuongezea uchungu badala ya kumpa furaha. Hii inaonyesha kuwa tendo hili si adilifu. Msimulizi anaeleza athari hii ya wizi katika ubeti wa pili kwa kusema kuwa:

> Siku ya kesi watu wengi walifika
> Kusikiliza hiyo hukumu yake
> Miaka saba kazi ngumu gerezani
> Ujana wake waishia kifungoni.

Kwa mujibu wa sheria za nchi ya Kenya, tendo la kuiba halikubaliki/ si adilifu hivyo ukilitenda, utakuwa umeivunja sheria hii. Ufanyapo hivyo, athari yake ni adhabu ambayo ni kutiwa gerezani na kupewa kazi ngumu. Aidha, uchungu huu umetokana na kutofuata mojawapo ya sheria katika dini ya kikristo ambayo inakataza kuiba. Katika ubeti wa tatu, msimulizi anasema kuwa "mali ya wizi haina baraka" kumaanisha kuwa mali ya wizi ina laana itokayo kwa Mungu. Kutekeleza wizi ni kuvunja mojawapo ya sheria za Mungu zilizo katika dini ya Kikristo ambayo inakataza wakristo kuiba. Unapoiba basi unapata laana kutoka kwa Mungu, jambo liletalo uchungu kwa mhusika.

Kwa mujibu wa nadharia ya unufaishaji hasi, binadamu hufanya maamuzi ya kutekeleza tendo fulani kwa kutawaliwa na kigezo cha uchungu au furaha. Katika wimbo huu, mhusika anaamua kuuza mali ya wizi kutokana na tamaa ya faida. Lengo lake mhusika lilikuwa kupata faida kutokana na mali ya wizi. Hili linaonyesha kuwa alitamani sana kupata pesa kwa haraka ili atajirike hivyo apate furaha. Mali nyingi/ utajiri humpa furaha kwa sababu pesa humpa mtu uwezo wa kutoa amri kwa watu katika jamii na kutumikiwa na watu. Uamuzi wa mhusika wa kununua mali ya wizi kisha kuiuza kwa hivyo ulitawaliwa na kigezo cha furaha kwani, alitaka kupata faida nyingi na kwa haraka ili apate furaha.

Katika ubeti wa pili tuliotangulia kuuunukuu, msimulizi anaeleza kuwa ni watu wengi sana waliofika katika kesi ya kijana mhusika ili kuisikiliza hukumu yake. Hili lina maana kuwa ni watu wengi waliokuwa wamekerwa au wameathiriwa na hili tendo la mhusika la kuivunja sheria kwa kushiriki katika wizi. Kwa hivyo, walioathiriwa na tendo la mhusika la kushiriki katika wizi ni jamii pamoja na kijana mwenyewe maanake aliathiriwa kwa kufungwa gerezani na kupewa kazi ngumu.

Kwa mujibu wa nadharia ya unufaishaji hasi, vigezo vinavyopaswa kutumiwa katika kupima kiasi cha uchungu upunguzwao/ kuongezwa na tendo ni kiwango, muda, ukali na uwezekano. Kigezo cha kiwango kinarejelea idadi ya watu walioathiriwa na tendo husika. Katika ubeti tulionukuu wa pili, tunaelezwa kuwa ni watu wengi wanaoathiriwa na tendo la mhusika la kuwauzia mali ya wizi, idadi inayodhihirika kupitia kwa watu wengi wanaofika mahakamani kusikiliza hukumu itakayotolewa kwa mhusika wakitarajia kuwa haki itatendeka ya mhusika kufungwa gerezani. Kigezo kingine kinachodhihirika katika ubeti huu ni muda ambao uchungu utapunguzwa/ kuongezwa. Tendo hili la kuuza bidhaa za wizi linaongeza uchungu kwa mhusika

mwenyewe kwa kipindi kirefu kwani anafungwa gerezani kwa miaka saba huku akifanya kazi ngumu. Huu ni muda mrefu kwa mhusika hasa kwa kuwa gerezani ambamo hana uhuru wa kufanya atakacho kisha anapewa kazi ngumu. Pia inaonekana kuwa jamii imeathiriwa na tendo hili la mhusika la kuwauzia bidhaa za wizi kwa muda mrefu. Hii ni kwa sababu wanaonekana wamekerwa na kuchoshwa sana na mhusika ndiposa wanafika mahakamani kwa wingi.

Kigezo kinginecho kinachodhihirika katika ubeti huu ni ukali. Uchungu anaohisi mhusika unaongezeka kwa kiwango cha juu kutokana na tendo lake la kuuza bidhaa za wizi kwani badala ya kupata pesa nyingi alizotarajia na kwa haraka, anahukumiwa kwa miaka saba na kupewa kazi ngumu. Vilevile, mtunzi anasema kuwa ujana wa mhusika utaishia gerezani kumaanisha kuwa hataweza kufurahia ujana wake kwani utaishia gerezani huku akiutumia kufanya kazi ngumu gerezani. Msimulizi katika ubeti wa tatu anasema kuwa "Mali ya wizi wala haina baraka" kumaanisha kuwa mali ya wizi huleta laana.

Kuna uwezekano mkubwa kuwa unapoiba, utapata laana ambayo humfanya mhusika kupata uchungu maishani mwake. Sheria za dini kama vile ya Kikristo zinakataza wizi ndiposa msimulizi anasema kuwa mali ya wizi haina baraka. Kuiba ni kuvunja mojawapo ya amri kumi za Mungu zilizoko katika dini ya Kikristo.

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa tendo hili la wizi linaongezea wahusika huzuni sana na kwa muda ulio mrefu. Aidha, tendo hili linaathiri watu wengi yaani mhusika na wanajamii. Hili linadhihirisha kuwa tendo la wizi si adilifu. Vilevile, asasi ya dini na sheria inakataza wizi kuonyesha kuwa si tendo adilifu. Joseph Ngala kwa hivyo anawahimiza wanajamii kufuata/ kutii sheria ya kutoshiriki katika wizi, kwani kufanya hivi kutawapunguzia uchungu wala si kuuongeza. Haya ndiyo maadili anayosisitiza katika wimbo huu.

### 3.2 KUTOKUWA NA TAMAA

Msanii Joseph Ngala anahimiza wanajamii kutokuwa na tamaa hasa ya mali au pesa. Katika wimbo tuliotangulia kuchambua, msanii huyu anaeleza katika kibwagizo kuwa mhusika anayemzungumziwa anajipata gerezani kutokana na tamaa ya faida ya wizi. Hili linajitokeza katika kibwagizo ambapo anasema kuwa:

> Ooh mama nasikitika
>
> Kijana mwema kama huyu kutupwa gerezani
>
> Kwa tamaa ya faida ya wizi
>
> Ooh mama nasikitika x2

Tendo hili la kuwa na tamaa ya pesa linaweza likatathminiwa kwa misingi ya uadilifu kwa sababu zifuatazo. Kwanza, kwa kutumia kigezo cha ubinadamu, mhusika aliye na tamaa ya pesa ni mtu anayetarajiwa kuwa na uwezo wa kutofautisha lililo baya na zuri na kuthibiti hisia zake za tamaa ya pesa. Aidha, kijana huyu ana uhuru wa kuchagua aongozwe na tamaa yake ya pesa za haraka au avumilie azitafute pesa kwa njia iliyo ya halali. Kwa kuangalia kigezo cha fikra zilizo na urazini, mhusika anapoamua kukubali kutawaliwa na hisia zake za tamaa ya mali inayomfanya kushiriki katika wizi, alikuwa katika ufahamu kamili hivyo tunatarajia aweze kufanya uamuzi mwafaka wa kutokuwa na tamaa.  Hii inadhihirisha kuwa tendo hili linaweza likabainishwa kama ni adilifu au si adilifu.

Kichochea kikuu cha mhusika cha kuwa na tamaa ya pesa ni kupunguza uchungu anaohisi kwa kutokuwa na pesa maanake anatarajia kuwa akiuza mali ya wizi atapata faida kubwa/ pesa nyingi. Anatarajia kuwa na pesa nyingi kutampunguzia uchungu. Hata hivyo, kinyume chake kinatokea kwani anashikwa na kutiwa gerezani hivyo kuongezea uchungu alionao badala ya kuupunguzia.

Walioathiriwa na tendo la mhusika la kuwa na tamaa ni jamii na pia mhusika. Katika wimbo huu wa *Fuateni Mambo ya Sheria*, jamii imekerwa sana na tendo la mhusika la kuwaibia kutokana na tamaa aliyo nayo ya pesa. Mhusika mwenyewe anaathiriwa kwani anafungwa gerezani kwa miaka saba huku akifanya kazi ngumu.

Tendo la mhusika la kuwa na tamaa ya pesa linamfanya ashiriki katika wizi. Tendo hili linamuongezea mhusika uchungu anaohisi wa kutokuwa na pesa kwa kuwa anafungwa gerezani na kupewa kazi ngumu. Hii ina maana kuwa tendo hili la kuwa na tamaa ya pesa si adilifu kwani linamuongezea mhusika uchungu badala ya kuupunguza.

Kwa kutumia vigezo vya kupima kiasi cha uchungu uongezwao/ upunguzwao na tendo fulani, tendo la kuwa na tamaa ya pesa lina athari zifuatazo. Kwa kuangalia kigezo cha ukali, uchungu anaohisi mhusika unaongezeka kwa kiwango cha juu kwani anafungwa gerezani kwa muda mrefu huku akifanya kazi nzito. Pia anahisi uchungu mwingi kwani hataweza kufurahia ujana wake kwa sababu msimulizi anaeleza kuwa utaishia gerezani. Kwa kuangalia kigezo cha muda, mhusika atahisi ongezeko la uchungu kwa muda mrefu kwani atafungwa kwa miaka saba. Aidha, kuna uwezekano mkubwa kuwa tendo la mhusika la kuiba litamuongezea huzuni maishani mwake kwani mtunzi anaeleza kuwa mali ya kuiba haina baraka kumaanisha kuwa unapoiba, utapata laana. Hatimaye, ni idadi kubwa ya watu walioathiriwa na tendo hili kwani linaathiri mhusika mwenyewe na pia jamii.

Maelezo haya yanathibitisha kuwa tendo la kuwa na tamaa ya mali ni tendo lisilo adilifu kwani linaongeza uchungu anaohisi mhusika na kwa muda mrefu ndiposa msanii anatumia wimbo huu kuhimiza jamii kutokuwa na tamaa ya mali na ya kupata vitu kwa urahisi bila kuvifanyia kazi. Tufanyapo hivyo basi, uchungu tunaohisi utapungua kumaanisha kuwa tendo la kutokuwa na tamaa ya mali ni tendo adilifu.

Tamaa nyingine anayozungumzia mwandishi ni tamaa ya raha za dunia. Anaeleza haya katika wimbo wa *Mwana Mpotevu*. Msanii anaonya jamii kuhusu kukimbilia raha za dunia. Anawahimiza wanajamii wawe na sifa ya kuchukulia mambo kwa utaratibu wala si kuyapapia.

Msanii anaeleza yote haya katika wimbo wa *Mwana Mpotevu*; usimulizi anaoutoa ni sawa na ule wa kisa cha mwana mpotevu katika Biblia (Good News: 1976). Kisa hiki husimulia kuhusu kijana aliyekuwa kitinda mimba na aliyeamua kuitisha urithi wake kutoka kwa babake. Baada ya kupewa urithi wake ambao ulikuwa ni mali, aliamua kuiuza na kuenda nchi ya mbali. Alipofika huko, alijihusisha na anasa za dunia, jambo lililomfanya afuje pesa alizokuwa nazo.

Kwa bahati mbaya, ukame ulitokea nchini mle hivyo alitumia pesa zote alizokuwa nazo. Ilimbidi afanye kazi katika shamba la mkaaji mmoja nchini mle ambapo aliajiriwa kama mchungaji

nguruwe. Alipokuwa kule, alihisi njaa sana maanake hakuna mtu yeyote aliyeshughulika kumpa chakula hadi akatamani ale chakula cha nguruwe. Akiwa katika hali hii, alikumbuka wafanyakazi wa babake ambao hupewa chakula kingi zaidi ya kile wanachohitaji. Aliona afadhali arudi nyumbani awe mmojawapo wa wafanyakazi wa babake. Alipanga kurudi kisha aombe msamaha kwa babake maanake aliona amemkosea yeye na hata Mungu. Anaporudi, punde tu babake alipomuona alimhurumia sana kutokana na hali yake mbaya. Alimkaribisha na kumkumbatia kisha anaagiza achinjiwe ndama. Kisa hiki kinaonyesha kuwa dini ya Kikristo inaonya wakristo kutokuwa na tamaa ya raha za dunia kwani kufanya hivyo husababisha maangamizo.

Joseph Ngala basi anasimulia kuhusu mwana mpotevu ambaye alitamani ya dunia sana hadi akatoroka nyumbani. Wazazi kwa kawaida, kutokana na tajriba yao ya maisha wanafahamu mengi kuhusu dunia, hivyo hujaribu kwa vyovyote vile kumkanya mtoto wao kuhusu kuingilia raha za dunia. Vijana huhisi kuwa wako katika upeo wa maisha yao na kamwe huwa hawataki maisha yao yaingiliwe na mtu yeyote. Hujiona wana uwezo wa kukabiliana na lolote linalowapata. Hata hivyo, wengi huishia katika hali ya laiti ningalijua. Hii ndio maana mhusika anatoroka nyumbani ili aishi atakavyo bila kuingiliwa na mtu yeyote. Hata hivyo, anapata matatizo chungu nzima kama anavyoeleza msimulizi katika mshororo unaosema kuwa, “amepigwa na dunia, pole mpeni.”

Tendo hili la tamaa ya raha za dunia linatimiza matakwa ya kutathminiwa katika misingi ya maadili. Hii ni kwa sababu kwanza, tendo hili linahusu binadamu ambaye ni kijana tunayetarajia awe na uwezo wa kufanya uamuzi ufaao wa kukaa nyumbani au kutoroka. Pili, kijana huyu hakufukuzwa nyumbani kwa hivyo alikuwa na uhuru wa kuchagua akae kule au atoroke. Tatu, kijana huyu ana fikra zilizo na urazini zinazopaswa kumwezesha kufanya uamuzi ufaao yaani, alipaswa kutathmini ikiwa ni makosa kwake yeye kutoroka nyumbani au la.

Baada ya mhusika kutoroka nyumbani kama tunavyoelezwa katika ubeti wa pili, hakupata raha za dunia kama alivyofikiria. Hii inaonyesha kuwa alipotoroka nyumbani alikuwa na pesa na labda alidhani kuwa hazitakwisha lakini hatimaye zinamwishia hadi anashindwa kujinunulia mavazi. Hili linajitokeza katika ubeti wa pili ambapo msimulizi anasema kuwa:

Akamshika mkono, kumpeleka za nyumbani

Nguo zimemchanika, raha za dunia

Baba kamwe hakujali, alimkumbatia

Na kisha akamwambia, kwangu ni kwako

Mwanangu usihuzunike, hii ni nyumba yako.

Wimbo huu unadhihirisha kuwa tendo la mhusika la kutoroka nyumbani kutokana na kuwa na tamaa ya raha za dunia kunatawaliwa na kigezo cha furaha. Hii ni kwa sababu kuna uwezekano kuwa sababu kuu ya mhusika kutoroka nyumbani ni kupata uhuru wa kula raha anavyotaka bila kuingiliwa na wazazi wake. Anapochukua hatua hii ya kutoroka nyumbani, anadhani kuwa atafurahi sana lakini raha anazokimbilia zinamwathiri kiasi cha kushindwa kujinunulia mavazi.

Suala lingine linalodhihirika katika wimbo huu ni kuwa, tamaa ya raha za dunia aliyonayo mhusika na inayomfanya kutoroka nyumbani inamwathiri yeye na pia wazazi wake. Mhusika anapotoroka nyumbani, anarandaranda kila mahali akila raha za dunia lakini hatimaye anaishiwa na pesa kiasi cha kumfanya akose hata mavazi. Anapata shida nyingi hadi anaona afadhali arudi nyumbani. Anarudi nyumbani akiwa mnyonge na akiwa amevaa mararu. Hili linaonyesha kuwa alipata athari mbaya kinyume na alivyotarajia. Wazazi nao wanaathiriwa kwani mhusika anapotoroka, bila shaka wanabaki katika hali ya majonzi kwa kumpoteza mtoto wao, wasijue hatimaye ama atarudi au hatarudi. Hii ndio maana mhusika anaporudi, wazazi wanampokea kwa mikono miwili na kwa raha tele.

Tendo la tamaa ya raha za dunia linamwongezea mhusika uchungu na pia wazazi wa mhusika kwa hivyo si tendo adilifu. Mhusika anatoroka nyumbani ili kuepukana na uchungu anaohisi wa kukatazwa kuponda raha atakavyo. Hata hivyo, anapotoroka anapata shida zaidi hadi inamlazimu kuvaa mararu. Anarudi akiwa mwenye huzuni tele. Wazazi wake nao wanahuzunika zaidi kwa kumpoteza mtoto wao anapotoroka ndiposa wanafurahi sana anaporudi. Tendo hili kwa hivyo si adilifu maanake linaongeza uchungu mwingi kwa kijana na wazazi.

Kwa kutumia vigezo vya kuamua iwapo tendo ni adilifu au si adilifu kwa kupima uchungu uongezwao/ upunguzwao na tendo fulani kwa mujibu wa nadharia ya unufaishaji hasi, tendo la

kuwa na tamaa ya raha za dunia lina athari zifuatazo. Kwa kuzingatia kigezo cha ukali unaoletwa na tendo la tamaa ya raha za dunia tunapata kuwa, mhusika anapata ongezeko la uchungu mwingi kutokana na matatizo yanayomkumba baada ya kutoroka nyumbani akikimbilia raha za dunia. Anarudi nyumbani akiwa amevaa mararu kuonyesha kuwa pesa zilimwishia kiasi cha kutoweza kujinunulia hata nguo. Afikapo mlangoni analia kutokana na majuto aliyonayo kwa kutoroka nyumbani. Aidha, wazazi wanahisi uchungu mwingi kwa kumwona mtoto wao akipotoka ndiposa wanajaribu kumrekebisha lakini kijana huyu anapotoroka wanahisi uchungu zaidi maanake hawajui ama yu hai au amefariki. Hii ndio maana anaporudi wanafurahi sana na kumpokea kwa mikono miwili ingawa aliwakosea.

Kutoroka kwa mhusika nyumbani ili aende kuponda raha kunamwathiri kwa muda mrefu maanake msanii anasema kuwa amerandaranda duniani lakini leo amerudi. Anarudi akiwa katika hali ya kusikitisha kwani anarudi akiwa amevaa mararu kuonyesha kuwa amepata shida kwa muda mrefu. Anaporudi, anaangua kilio afikapo mlangoni kuonyesha kuwa ameteseka sana na kwa muda mrefu, mateso yaliyomfanya aone kuwa aliwakosea wazazi wake na Mungu. Kipindi hicho ambacho mhusika aliteseka ndicho nao wazazi waliteseka kwani hawakuwa na ufahamu wa ikiwa mtoto wao yu hai ama amefariki.

Kuna uwezekano kuwa kitendo cha mhusika cha kutoka nyumbani bila idhini ya wazazi wake ili kusaka raha kitasababisha shida/ huzuni zaidi. Mhusika anasema kuwa amewakosea wazazi wake na pia Mungu kwani anakataa kuishi nao na kufuata amri zao kwake ndipo anatoroka nyumbani. Kama tulivyoeleza katika sura ya pili, kuna uhusiano mkubwa kati ya maadili na dini. Mojawapo ya amri kumi za Mungu katika Biblia ni kuwatii wazazi ili siku zako za kuishi duniani ziongezeke. Wakristo wanaamini kuwa unapotii amri hii, utapata baraka lakini usipofanya hivyo ina maana kuwa utakosa baraka/ utapata laana. Hii ina maana kuwa kuna uwezekano mkubwa wa mhusika kupata huzuni zaidi kutokana na laana atakayopata kwa kutotii wazazi wake na kutoroka nyumbani.

Vigezo hivi vinadhihirisha wazi kuwa tendo la mhusika la tamaa ya raha za dunia linasababisha ongezeko la huzuni kwa kiwango cha juu kwake mhusika na wazazi wake. Walioathiriwa ni watu watatu (mhusika na wazazi) kisha wanahisi ongezeko la huzuni kwa muda mrefu. Hili ni thibitisho kuwa tendo la kuwa na tamaa ya raha za dunia si adilifu. Sababu za kidini hasa ya Kikristo kama tulivyoeleza vilevile zinadhihirisha kuwa tendo hili si adilifu. Hii ndio maana

mtunzi anaihimiza jamii kutenda kinyume chake ambacho ni kutokuwa na tamaa ya raha za dunia kwani kutawapunguzi huzuni waliyonayo hivyo ndilo tendo adilifu.

### 3.3 KUSIKILIZA MAWAIDHA YA WAKUU/ WAZAZI

Joseph Ngala kupitia nyimbo zake anawahimiza wanajamii, hasa vijana kusikiliza mawaidha wanayopewa na wakuu wao kwani asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Katika jamii nyingi barani Afrika, wazee/ wazazi ni mojawapo wa wale wanaotumika kuhakikisha kuwa maadili katika jamii yamefuatwa. Vijana wengi hasa wanapobaleghe hutaka sana kuwa na uhuru wa kujitawala bila kuingiliwa na mtu yeyote. Wao hukaidi wanayoambiwa na wazazi wao bila kufahamu kuwa kutokana na tajriba yao ya maisha, wanayowaambia huwa yana umuhimu mkubwa katika kuyaelekeza maisha yao.

Hobhous (1922) akimnukuu Rousseau anasema kuwa mtu huzaliwa akiwa huru lakini kila wakati yuko katika minyororo kwa hivyo kila mara hujaribu kujiweka huru. Uhuru huu unahusu mamlaka au nafasi, ambayo tunaweza tukaitumia vizuri au vibaya. Hata hivyo, ni kwa kuitumia nafasi hii vizuri ndipo tu ustawi wa binadamu hutimilika. Katika kutamani uhuru, binadamu hujidanganya katika fikra zake kuwa ana nguvu zisizo na kipimo ambazo zitamwezesha kufanya lolote atakalo. Binadamu hutafuta uhuru ili kuepukana na vizuizi vinavyomzuia kufanya atakavyo kulingana na uamuzi wake. Ni jukumu la kila mtu basi kuwa na hiari ya kutenda linalofaa kwa kupima iwapo tendo hilo litakuwa la kuleta furaha au uchungu. Iwapo litaleta furaha basi tendo hilo ni adilifu lakini iwapo litaleta uchungu, litakuwa si adilifu.

Katika wimbo wa *Ndivyo Ilivyo Dunia,* msanii anasimulia kisa cha mwenzake aliyejaribu kumpa mawaidha lakini akakosa kutilia maanani aliyomwambia. Anadokeza kuwa alimsihi kuachana na mpenziwe (ambaye inaonekana kuwa alikuwa anamchumbia) maanake alifahamu kuwa anamchezea tu. Hili linadhihirika katika ubeti wa tatu unaosema kuwa:

> Nilijua akudanganya, nikajaribu kukukanya
>
> Huwezi kunilaumu, kwa yalokupata
>
> Na laiti ungelijua, ungefuata yangu

Anaendelea kueleza katika wimbo huu kuwa ndivyo ilivyo dunia, akikua atayajua mengi ambayo hajayafahamu. Msimulizi anadokeza hili katika ubeti wa nne kwa kusema kuwa:

Nilipokudokeza, mwenzangu ukanipuuza
Hivi sasa walia, itafaa nini
Ndivyo ilivyo dunia, kua uone mengi

Maelezo katika ubeti huu yanadhihirisha kuwa anayetoa mawaidha ni mzee maanake ameifahamu dunia vyema kutokana na tajriba yake ya maisha. Hii ndio maana anasema kuwa ndivyo ilivyo dunia, kuwa kuna asali na shubiri hivyo lazima uwe makini katika kung'amua ni yepi mazuri na ni yepi mabaya. Hata hivyo, mzazi wa mhusika anachukua jukumu la kumshauri kuhusu yanayomzingira lakini mhusika anayapuuza. Alikataa kusikiliza ushauri aliopewa kisha akaendelea kuyatenda kwa siri lakini mwishowe yalichipuka na kuwa dhahiri. Kama tulivyoeleza hapo awali, vijana wakuapo hutaka kuishi maisha huru bila kuingiliwa na mtu yeyote huku wakiwa na fikra danganyifu kuwa wana uwezo wa kukabili yoyote yanayowapata. Msimulizi anaeleza hili katika ubeti ufuatao kwa kusema kuwa:

Uliyachukua siri, hivi leo yako dhahiri
Asosikia la mkuu, huvunjika guu
Langu ni kukupa pole, ilivyo dunia

Kulingana na Dobeljuh (2006), tendo linalojitokeza katika wimbo huu la kusikiliza mawaidha ya wakuu linaweza kutathminiwa katika misingi ya maadili yaani, ikiwa ni adilifu au si adilifu. Hii ni kwa sababu linatosheleza vigezo vinavyotumika kufanya hivyo. Katika kigezo cha kwanza cha ubinadamu, mhusika anayezungumziwa katika wimbo huu ni binadamu aliye na uwezo wa kutathmini uhusiano wake na mpenziwe na kubaini iwapo rafikiye anamhadaa au la. Pili, mhusika alikuwa na uhuru wa kuchagua aendelee na uhusiano aliokuwa nao na mpenziwe licha ya kukanywa asifanye hivyo au akatize uhusiano ule. Tatu, mhusika yuko katika fikra zilizo na urazini za kumwezesha kung'amua kama rafikiye anampenda kwa mapenzi ya dhati au ni kumhadaa tu. Mhusika alikuwa na ufahamu ulio kamili.

Tendo la mhusika la kutosikiliza mawaidha aliyopewa linatawaliwa na kigezo cha kupunguza huzuni. Uhusiano aliokuwa nao mhusika na mpenziwe unaonekana ulimpunguzia huzuni ya kuwa pweke, hali iliyompumbaza asione kuwa rafikiye alikuwa anamhadaa. Mhusika hakutaka kumwacha rafikiye kama alivyoshauriwa kwa sababu aliona atabaki pweke. Hii ndio maana anaposhauriwa kumuacha, anakataa na kuendelea na uhusiano ule kwa siri kumaanisha kuwa

alikuwa ameridhishwa sana na mpenziwe. Hatimaye anapoachwa na mpenziwe, analia sana na kuhuzunika kuonyesha kuwa alimpenda sana hivyo urafiki ule ulimpunguzia huzuni.

Katika muktadha wa wimbo huu, mhusika tu ndiye anayeathiriwa na tendo la kutosikiliza mawaidha aliyopewa ya kuachana na mpenziwe. Anapata ongezeko la huzuni maanake anapoachwa analia sana na kujawa na majuto ya kukaidi ushauri aliokuwa amepewa. Aliyemshauri anasema kuwa alitimiza wajibu wake wa kumshauri kwa hivyo analoweza kufanya tu ni kumpa pole. Mhusika anapoachwa anabaki akilia huku akijuta kwa kutosikiliza ushauri aliopewa. Tendo hili linampa mhusika huzuni zaidi kwa hivyo ni tendo lisilo adilifu. Msimulizi anaeleza hili katika ubeti wa kwanza na wa tatu kwa kudokeza kuwa:

Nilipokudokeza, mwenzangu ukanipuuza
Hivi sasa walia, itafaa nini
Ndivyo ilivyo dunia, kua uone mengi.

Hivi umekwama, wabaki kushika tama
Ijapokuwa nakwambia, nakuhurumia
Ndivyo ilivyo dunia, ukae ukijua.

Kwa kutumia vigezo vya kuamua iwapo tendo ni adilifu au si adilifu kwa kupima uchungu uongezwao/ upunguzwao na tendo fulani kwa mujibu wa nadharia ya unufaishaji hasi, tendo la kutosikiliza mawaidha ya wakuu lina athari zifuatazo. Kwa kuangazia kigezo cha ukali, mhusika anahisi ongezeko la uchungu la kiasi cha juu kutokana na kuhadaiwa kisha kuachwa na aliyemchukulia kuwa mpenziwe. Mtunzi anaeleza kuwa mhusika baada ya kuachwa analia sana na kujuta kwani alikanywa lakini akapuuza. Katika kigezo cha muda, kulingana na msimulizi inaonekana kuwa mhusika hajakaa kwa muda mrefu baada ya kuachwa na mpenziwe aliyemhadaa. Mzazi katika wimbo huu anasema kuwa alimkanya mhusika lakini akakosa kumsikiliza kwa hivyo sasa yualia na kujuta kumaanisha kuwa muda mrefu haujapita baada ya mhusika kuachwa. Hii inaonyesha kuwa muda ambao mhusika amehisi ongezeko la uchungu wa kuachwa na mpenziwe si mrefu.

Katika kigezo cha uwezekano, inabainika kuwa kuna uwezekano wa kuwa tendo la mhusika la kutosikiliza mawaidha anayopewa na mzazi wake kutamwongezea huzuni. Hii ni kwa sababu mzazi wa mhusika anamtahadharisha kuhusu uhusiano alionao kwani, kutokana na tajriba aliyonayo ya maisha aliweza kung'amua kuwa mpenziwe mhusika alikuwa anamdanganya tu. Hii ndio maana mzazi anasema kuwa lake tu ni kumpa pole maanake alimkanya lakini hakumsikiliza. Kwa kuangazia kiwango/ idadi ya walioathiriwa, mhusika tu ndiye anayeathiriwa na tendo lake la kutosikiliza mawaidha aliyopewa na mzaziwe. Mzaziwe anasema kuwa lake tu ni kumpa pole lakini hakuna analoweza kufanya zaidi ya hilo kwani alimkanya lakini hakumsikiliza.

Kutokana na maelezo haya, tendo la kutosikiliza mawaidha ya wazazi kunaleta ongezeko la uchungu kwa mhusika kwa hivyo ni tendo lisilo adilifu. Mwimbaji kwa hivyo anakusudia kutoa funzo kuwa, ni vyema kwa vijana kusikiliza mawaidha wapewayo na wakuu ambao wana tajriba pevu ya maisha maanake wakifanya hivyo, uchungu wanaohisi wa kukatazwa kuponda raha za dunia utapungua kumaanisha kuwa tendo hilo ndilo adilifu.

Maudhui haya ya kusikiliza mawaidha ya wakuu pia yanazungumziwa katika wimbo wa *Nisikilize Mwanangu.* Msimulizi katika wimbo huu anamhimiza mhusika (mwana) kusikiliza anayomweleza maanake angali mchanga na mengi ya dunia hajayajua. Anamwambia kuwa aendako kuna mengi: pepo zavuma , kuna jua hata na mvua kumaanisha kuwa kuna mengi ya hatari yatakayomkabili asipokuwa mwangalifu. Mzazi anamtahadharisha mwanawe kuwa asiposikiliza mawaidha anayompa ya kuwa mwangalifu, atapigwa na dunia kisha aanze kujuta. Hii ndio maana anamwambia kuwa asijigambe kwani binadamu ni kama maua; asipomakinika atapigwa na dunia kisha kusinyaa. Mzazi vilevile katika ubeti wa kwanza anamweleza mtotowe kuwa asiposikiliza ushauri wake hatimaye atakuja kujuta lakini atakuwa amechelewa sana. Hii ni kwa sababu siku za ujana zikipita hazirudi. Haya yanajitokeza katika ubeti wa kwanza na wa pili ambapo msimulizi anasema kuwa:

Ewe kijana, hivi sasa wakua
Watoka mbali, mzigo hujautua
Pia wendapo mwanangu, bado hujakujua
Nisikize basi, machache ntakwambia

Huko uendako, ndiko kwenye dunia
Pepo zavuma, na jua hata mvua
Na ukifurahi leo, lazima kuelewa
Vimbele vyakungojea.
Sote twajua, tuko kama maua
Piga kifua, kesho waanza fifia
Nakisha wafikiria, laiti ungejua
Heri ungejua, sori umeshachelewa
Washika tama, hapo huna la kufanya
Siku za raha, ndio hazirudi tena
Na hata hivi nasema, kisha wanisikia
Najua najisumbua.

Katika ubeti huu, vigezo vya kuweza kulitathmini tendo hili katika misingi ya maadili vinajitokeza. Katika kigezo cha kwanza cha ubinadamu tunaona kuwa, mhusika katika wimbo huu ni kijana ambaye ana uwezo wa kufikiria kama binadamu na kuweza kufanya uamuzi ufaao kuhusu analoshauriwa la kutopapia maisha kwani yatamwangamiza. Pili, mhusika ana uhuru wa kuamua kusikiliza anayoshauriwa ya kutokimbilia raha za dunia na kufanya vituko vinavyomhuzunisha mzaziwe. Tatu, mhusika yuko na fikra zilizo na urazini za kumwezesha kufanya uamuzi mwafaka wa kusikiliza ushauri anaopewa kwani asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Tendo la mhusika la kukimbilia raha za dunia bila kusikiliza mawaidha anayopewa linatawaliwa na kigezo cha furaha. Msimulizi anasema kuwa mhusika ambaye ni kijana anataka sana kuikimbilia dunia lakini hajui kuwa anakokimbilia kuna asali na pia shubiri "Huko uendako ndiko kwenye dunia; pepo zavuma na jua hata mvua." Anamwambia kuwa anataka kula raha sana akiwa kijana lakini akiupoteza ujana wake hautarudi. Mhusika anapiga kifua kuonyesha kwamba anajigamba kuwa anaweza akafanya atakalo bila kuingiliwa na mtu yeyote lakini mzazi anamshauri kuwa binadamu ni kama maua, ale raha tu lakini hatimaye atasinyaa. Hili linaonyesha kuwa mhusika hakutaka kusikiliza mawaidha aliyopewa kwa kutaka kusaka raha akiwa angali kijana.

Mhusika kwa kutosikiliza mawaidha aliyopewa hatimaye kutamwathiri yeye na mzazi wake. Msimulizi anamuonya mhusika kuwa pale machozi ya mzaziwe yatamdondoka ajue ataanguka. Hii ina maana kuwa mzaziwe alipata huzuni zaidi kutokana na mhusika kutomsikiliza. Mhusika naye ataathirika maanake mzazi wake anamweleza kuwa asiposikiliza kwamba anapaswa kutahadhari maishani, hatimaye atakuja kushika tama kwa majuto. Hii ni kwa sababu atakuwa ameharibu ujana wake kwani ukipita haurudi. Vilevile, mhusika anatahadharishwa na msimulizi kuwa akiendelea na vituko alivyo navyo kisha vimfanye mzaziwe alie, ataanguka na mengi ya dunia yatampata. Hii ina maana kuwa mhusika atapata huzuni tele hasa kutokana na laana ya kutotii mzaziwe. Hili linajitokeza katika ubeti ufuatao ambapo msimulizi aneleza kuwa:

Mzazi yule, ndiye aliyekulea
Imani yake, lake lishamwondokea
Bali kwa vituko vyako, lawama za dunia
Akifikiria, mara yuanza kulia
Machozi yale, yatakapomdondoka
Utaanguka, na mengi yatakufika
Na wengi watakusema, huku wasikitika
Nisikilize mwanangu.

Laana itakayompata mhusika kutokana na kutomtii mzaziwe hasa ni kulingana na tamaduni na imani ya kidini ya jamii nyingi za Afrika. Katika dini ya Kikristo kwa mfano, kati ya amri kumi za Mungu, amri iliyo na ahadi ni ile ya kuwatii wazazi. Ahadi yake ni kuwa siku zako za kuishi duniani zitaongezeka. Wakristo wanaamini kuwa ukifanya kinyume basi utapata laana kutoka kwa Mungu.

Dini huhusiana sana na maadili kama tulivyotangulia kueleza katika sura ya pili. Uhusiano kati ya dini na maadili ni kuwa nyanja nyingi za dini huelekeza kuhusu yaliyoadilifu na yasiyoadilifu ambayo huelekezwa kupitia kwa Biblia au Koran. Kwa mfano, katika dini ya Kikristo, amri kumi za Mungu huwa ni msingi wa sheria za maadili ambazo waumini wa dini ya Kikristo wanapaswa kufuata. Sheria nyingi za kidini huhimiza wanajamii kutekeleza yaliyo adilifu kwa mujibu wa jamii husika. Hata hivyo, haina maana kuwa yote ambayo sheria za kidini zinahimiza yatekelezwe ni adilifu au yote yaliyo adilifu yako katika dini.

Aidha, kuna uhusiano mkubwa kati ya dini na maadili hivi kwamba, tunaweza kudai kuwa kanuni za maadili hutokana na dini. Msingi wa uhusiano huu wa maadili na dini ni kuwa, watu wanapaswa kuishi maisha mazuri ambapo maisha mazuri huelezwa kulingana na mfumo wa wanayoamini. Kwa mfano, kulingana na dini ya Kikristo, mapenzi ya Mungu ndiyo mamlaka ya mwisho ya maadili; watu wanapaswa kufanya anayotaka Mungu na anayotaka Mungu ni mazuri. Atakayo Mungu kwetu hujulikana kupitia kwa Biblia au manabii ambao watu huamini wametumwa na Mungu. Wakristo pia huamini Mungu yuko juu akiangalia matendo yetu; hutuadhibu tunapokosea na pia kututuza tunapotenda mema. Huu ndio msingi ambao Joseph Ngala anatumia anaposema kuwa, kwa mhusika kutofuata anayoagizwa na mzaziwe na kumfanya alie basi ataanguka na mengi mabaya yatampata.

Matokeo ya mhusika kutosikiliza mawaidha anayopewa ni kuwa atapata ongezeko la uchungu. Mhusika anakasirika kwa kukatazwa kufanya anayotaka na mzaziwe, jambo linalompa uchungu. Msimulizi anaeleza kuwa mhusika asiposikiliza anayoelezwa hatimaye atakuja kujuta maanake atakuwa amepoteza ujana wake na atapata laana kwa kumfanya mzaziwe alie kutokana na vituko vyake. Hili litaongeza huzuni/ uchungu alionao. Huzuni hii itatokana na sababu za kidini na mhusika kukosa maadili. Tumeeleza kuwa amri ya Mungu katika dini ya Kikristo ni kutii wazazi kwa hivyo ukikosa kufanya hilo unapata laana. Mhusika naye anakosa kufanya uamuzi mwafaka wa kufuata yanayofaa ya kutii kwa hivyo atapata laana itakayomletea huzuni. Matokeo ya tendo hili ambayo ni ongezeko la huzuni yanadhihorisha kuwa tendo hili la kutosikiliza mawaidha si adilifu.

Kwa kutumia vigezo vya kuamua iwapo tendo ni adilifu au si adilifu kwa kupima uchungu uongezwao/ upunguzwao na tendo fulani kwa mujibu wa nadharia ya unufaishaji hasi, tendo la kutosikiliza mawaidha ya wakuu katika wimbo wa *Nisikilize Mwanangu* lina athari zifuatazo. Katika kigezo cha kiasi tunaelezwa kuwa, mhusika atapata uchungu zaidi ya ule anaohisi kwa kutazwa afanye atakalo, kwani atapata laana kutoka kwa Mungu itakayomfanya aanguke na kusemwa na wengi. Pia atapata majuto sana kwa kuwa atakuwa ameupoteza ujana wake. Msimulizi anasema kuwa mzazi atakapolia kutokana na vituko vya mhusika ambavyo havimridhishi ajue kuwa laana itampata. Hili linaonyesha kuwa mzazi anapata uchungu zaidi kutokana na vituko vya mtotowe. Muda ambao mhusika atahisi uchungu haujaelezwa maanake

wimbo huu unaeleza ushauri unaotolewa kwa kijana ambapo iwapo hatausikiliza ndipo athari zilizoelezwa zitatokea kuonyesha kuwa mhusika bado hajapatwa na athari hizo.

Katika kigezo cha uwezekano tunaona kuwa kuna uwezekano mkubwa wa tendo la kutosikiliza mawaidha ya wakuu kusababisha huzuni zaidi kwa mhusika na mzazi. Hili linadhihirika kupitia ushauri anaotoa msimulizi kuwa duniani kuna mazuri na mabaya kwa hivyo bila shaka usipokuwa mwangalifu kama alivyo mhusika, utaangamia. Pia anasema kuwa kutotii wazazi huleta laana. Mzazi pia hutarajia mtoto wake amtii kuonyesha kuwa akifanya kinyume, hilo litamhuzunisha mzazi. Kwa kuzingatia kigezo cha kiwango cha watakaoathiriwa na tendo hili la kutowasikiliza wakuu tunapata kuwa, mhusika pamoja na mzaziwe ndio watakaoathiriwa. Mhusika ataathiriwa maanake kama tulivyoeleza, asiposikiliza ushauri wa kuwa mwangalifu maishani, atapigwa na dunia, jambo litakalomfanya kusinyaa. Vilevile, atapatwa na huzuni na majuto kwani ataharibu ujana wake ambao ukipita haurudi. Mzazi vilevile anaathiriwa maanake atapatwa na huzuni kutokana na vituko vya mtotowe.

Vigezo hivi kwa hivyo vinadhihirisha kuwa tendo la kutotii wazazi linasababisha kiwango cha juu cha ongezeko la huzuni kwa wahusika kwa hivyo ni tendo lisilo adilifu. Msingi ambao tumeeleza wa dini pia unaonyesha kuwa tendo hili si adilifu. Msanii basi anashauri vijana kusikiliza mawaidha wapewayo na wazazi wao, wawaheshimu na kuwatii ili kuepukana na majuto na simanzi.

## 3.4 UPENDO

Maudhui mengine ya uadilifu yanayojitokeza katika baadhi ya nyimbo za Joseph Ngala ni ya upendo. Kwa mujibu wa kamusi ya Sosholojia ya Collins (1991), upendo ni hisia kama vile za huruma na wema kwa wengine. Pia ni mvuto unaohusisha watu wawili, mvuto wa kitu au jambo fulani. Upendo kama mojawapo ya kigezo cha maadili unahusu huruma na wema kwa watu wengine. Haya ni maadili yaliyo muhimu sana katika jamii kwani watu wanapopendana katika jamii huishi kwa amani. Hii ni kwa sababu unapompenda mtu utaepuka kumtendea mabaya yatakayomuudhi na badala yake, utamtendea yatakayomletea furaha. Kwa mujibu wa nadharia tunayoitumia ya unufaishaji, upendo tunaozungumzia ni ule ulio na dhana ya kuwa, “mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.” Hii ni kwa sababu unapojipenda, matendo unayotenda yatalenga kuleta furaha na kupunguza uchungu. Vilevile, upendapo wengine kwa

kiasi cha vile unajipenda mwenyewe, utawatendea matendo yanayolenga kusababisha furaha kwao wala si uchungu.

Joseph Ngala katika wimbo wa *Ndugu Tupendane* anasisitiza umuhimu wa upendo kati ya ndugu katika familia. Katika ubeti wa kwanza, anasema kuwa hakuna jambo zuri kama ndugu kupendana, upendo unaodhihirishwa kwa ndugu ni kila mara kujuliana hali na kuelewana. Hata kama watu wanaishi katika maeneo tofauti kijiografia, ni muhimu sana kwa watu hawa kujuliana hali. Msimulizi anaonyesha hili katika ubeti wa kwanza kwa kusema kuwa:

Kaka dada zangu, hii ni siku nzuri
Kupata nafasi, ya kuwaelezea
Hakuna jambo zuri, kama ndugu kupendana
Kumbukeni utotoni, tukiwa pamoja
Mola hupanga lake, kila mmoja akawa kwake
Na ni lazima sote, tujuliane hali
Kuna hili na lile, pale familia nzuri
Kuwa na maelewano, huleta baraka kote.

Anasema kuwa ingawa watu kwa wakati mmoja au mwingine hukosana, ni vizuri kusuluhisha tofauti hizi kila mara zinapotokea. Anawatahadharisha kuhusu mahasidi ambao huja kukosanisha watu hasa wanapoona wana ushirikiano mkubwa. Jambo zuri la kutenda kwa watu kama hawa ni kuwapuuza.

Katika wimbo huu, tumeeleza tendo la upendo katika misingi ya maadili maanake linatimiza matakwa ya kuweza kutathminiwa kama ni tendo adilifu au si adilifu. Kwa kuangazia kigezo cha kwanza, tendo hili linahusu binadamu ambao ni ndugu katika familia. Tunatarajia kwamba ndugu hawa wana uwezo wa kufanya uamuzi wa kupendana wala si kuchukiana. Aidha, ndugu hawa wana uhuru wa kuchagua kupendana au kuchukiana. Tatu, ndugu wanaozungumziwa wana fikra zilizo na urazini hivi kwamba wana uwezo wa kufanya uamuzi ulio mwafaka ambao ni wa kupendana.

Msimulizi anawahimiza ndugu katika familia kupendana ili kupata furaha. Hii ina maana kuwa uamuzi wa tendo la kupendana unatawaliwa na kigezo cha furaha. Msimulizi anaeleza katika ubeti wa kwanza kuwa watu wanapopendana hupata furaha kuu kutokana na baraka nyingi wanazopata. Hili linaonyesha kuwa matokeo ya tendo la kupendana yatawaathiri ndugu katika familia husika.

Tendo la upendo linapunguza uchungu unaotokana na kukumbwa na matatizo na kushindwa kuyasuluhisha kutokana na kutengana. Hii ni kwa sababu upendo huleta baraka na pia utawawezesha kusuluhisha tatizo lolote litakalowakabili kwa urahisi. Tendo hili kwa hivyo ni tendo lililo adilifu.

Kwa kutumia vigezo vya kuamua iwapo tendo ni adilifu au si adilifu kwa kupima uchungu uongezwao/ upunguzwao na tendo fulani, tendo la kuwa na upendo katika wimbo wa *Ndugu Tupendane* lina athari zifuatazo. Kwa kuangalia kigezo cha ukali/ kiwango cha nguvu ambacho wahusika watahisi kupunguzwa kwa huzuni, tunapata kuwa upendo unawapunguzia wahusika ambao ni ndugu uchungu mwingi kwani kama tulivyoeleza, wakipendana wataweza kusuluhisha tatizo lolote watakalopata kwa haraka. Muda ambao wahusika watahisi kupunguzwa kwa huzuni si dhahiri maanake msimulizi anatoa ushauri wa ndugu kupendana kwa kusema kuwa wakifanya hivyo watapata furaha kuonyesha kuwa tendo hilo halijatokea. Kuna uwezekano mkubwa kuwa tendo la upendo litapunguza huzuni maanake msimulizi anasema kuwa upendo huleta baraka.

Katika kigezo cha kiwango, wanaotarajiwa kuathiriwa na tendo la upendo ni ndugu katika familia husika. Msimulizi anasema kuwa upendo hupunguza huzuni kutokana na baraka watakayopata wahusika na kuweza kusuluhisha matatizo kwa haraka.

Vigezo hivi vinadhihirisha kuwa tendo la kupendana litapunguza huzuni/ uchungu kwa kiwango cha juu kwa wahusika ambao ni ndugu. Hii ina maana kuwa tendo la kuwa na upendo ni tendo adilifu.

### 3.5 UVUMILIVU

Uvumilivu ni uwezo wa kungojea mtu, kitu au jambo fulani bila kukasirika na kwa matumaini kuwa utapata matokeo mazuri. Kwa mujibu wa kamusi ya Kiingereza ya Collins (1979), uvumilivu ni uwezo wa kudhibiti hisia na mihemko na kuweza kuendelea kwa utulivu licha ya kukumbana na hali ngumu/ matatizo. Uvumilivu ni sifa ya kimaadili ambayo hutusaidia kutofanya maamuzi kwa haraka. Hutusaidia kukubali hali ya maisha hasa matatizo tunayokabiliana nayo katika maisha ya sasa tukitarajia kuwa siku za usoni zitakuwa bora. Mara nyingi mtu anapokumbwa na matatizo, watu wengi humshauri awe mvumilivu na mtulivu hata kabla ya kuwazia kuhusu suluhisho halisi la tatizo linalomkabili. Hii ni kwa sababu hali hii ya utulivu itamsaidia kuweza kufikiria vyema na kwa makini kuhusu suluhisho la tatizo linalomkabili badala ya kuwazia suluhisho kwa haraka ambalo litamletea madhara zaidi.

Ni muhimu kutaja kuwa uvumilivu ni maadili yanayothaminiwa sana katika dini nyingi kama vile ya Kikristo, Kiislamu, Kiyahudi, Kihindu n.k. Katika dini ya Kikristo kwa mfano, uvumilivu ni mojawapo ya matunda ya roho mtakatifu (Wagalatia 5:22-23). Wakristo huamini kuwa Yesu ni kielelezo cha uvumilivu kwani alivumilia mateso mengi kabla ya kifo chake. Katika sura ya pili, tulieleza kuwa dini na maadili ni masuala mawili ambayo hufungamana sana katika jamii yoyote ile.

Tendo la uvumilivu kwa hivyo ni adilifu na kukosa uvumilivu si uadilifu. Hii ni kwa sababu watu wasio na uvumilivu hukosa kuridhika, huwa na uwezekano wa hali ya juu ya kupata maradhi ya moyo kutokana na kukasirika, hujiuzulu kazini kwa haraka, huvunja urafiki na wengine haraka na pia hukosa msukumo kwa haraka wa kufikia lengo lao hasa wanapopata changamoto. Matokeo haya yote yanaleta uchungu kwa anayehusika kwa hivyo, hili ni tendo lisilo adilifu. Kwa upande mwingine, watu walio na uvumilivu hukosa kupata mfadhaiko kutokana na shida, hufurahia hatua ya kutimilika kwa jambo hata kama inachukua muda mrefu, huwa watulivu na wenye afya nzuri na hutimiza malengo yao kwa ufanisi wa hali ya juu. Haya yote ni matokeo yaletayo furaha kuonyesha kuwa, uvumilivu ni sifa adilifu. Kutokana na maendeleo ya kiteknolojia duniani, tunaweza kupata takribani kila kitu tunachohitaji kwa haraka, jambo ambalo linakisiwa kuwafanya watu kukosa subira ukilinganisha na awali.

Mwimbaji Joseph Ngala anazungumzia maudhui haya ya uvumilivu katika wimbo wake unaoitwa *Dada Vumilia*. Mhusika anahimizwa kuvumilia ingawa anapata dhiki sana. Anakumbushwa kuwa maishani, hakuna mtu asiyepatwa na shida kwa wakati mmoja au mwingine maanake maisha ni kupanda na kushuka. Yaani yana asali na shubiri. Wakati mmoja utafurahi lakini wakati mwingine upatwe na majonzi; hivyo ndivyo maisha yalivyo. Anamhimiza mhusika atulie, asife moyo katika ubeti wa kwanza anaposema kuwa:

Hebu dada vumilia, hayo ni mambo ya kawaida
Ingawa mimi najua, ile dhiki unapata wewe
Hakuna asiyesumbuka, kama si leo labda ni kesho
Utulize usifanye kufa, maisha ndivyo yalivyo.

Mwimbaji anaendelea kumhimiza mhusika kuwa kila lenye mwanzo huwa na mwisho kwa hivyo, anayopitia hatimaye yatafika mwisho na atakuja kuyasahau. Msimulizi anamkumbusha namna maisha yake yalivyokuwa kabla ya kupata shida alizonazo katika mshororo unaosema kuwa “ebu fikiria, kabla ya shida ulikuwaje.”

Katika wimbo huu, mwimbaji anatumia muktadha wa kidini kumueleza mhusika kuwa shida anazopitia ni majaribio tu ambayo hatimaye yataisha kwa hivyo, asife moyo. Si kwamba maisha yake yamefika mwisho. Katika dini ya Kikristo, wakristo huamini kuwa wanapopata shida huwa ni majaribio ya shetani na kwa wakati kama huo, wanapaswa kuvumilia, kuomba na kuwa na imani kuwa Mungu atawawezesha kuyashinda yote. Hii ndio sababu msimulizi anamfahamisha mhusika kuwa Mola anafahamu anayopitia kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao:

Yote hayo majaribu, mola mwenyewe anatambua
Hata hivyo usife moyo, sio mwisho wa maisha yako
Najua umejaribu, kwa mapenzi hata na riziki
Bahati haijasimama, iko siku utafaulu.

Maelezo haya ya wimbo huu yanadhihirisha kuwa tunaweza kulieleza tendo la kuvumilia katika msingi wa maadili. Hii ni kwa sababu linaafiki vigezo vinavyofanya tendo kuweza kuainishwa kama ni adilifu au si adilifu ambavyo ni tendo kuwa ni la kibinadamu, uhuru na mtendaji kuwa na fikra zilizo na urazini. Katika kigezo cha kwanza, mhusika anayehimizwa kuvumilia ni

binadamu tunayetarajia kuwa na uwezo wa kufikiria na kuweza kufanya uamuzi wa kutenda yafaayo ambayo ni kuvumilia wala si kukata tamaa. Pili, mhusika ana uhuru wa kuamua kuvumilia au kukata tamaa ndiposa msimulizi anamshauri afanye uamuzi wa kuvumilia anapomwambia kuwa "utulize usifanye kufa, maisha ndivyo yalivyo." Tatu, mhusika ana fikra zilizo na urazini kwa hivyo ana uwezo wa kufanya uamuzi ulio mwafaka ambao ni kuvumilia licha ya matatizo yanayomkumba. Msimulizi anamwambia mhusika afikirie kabla ya shida maisha yake yalikuwaje ili aweze kutathmini hali tofauti ambazo amepitia katika maisha yake ndiposa aone kuwa hata hali aliyonayo sasa itaisha. Hili linaonyesha kuwa alikuwa na fikra zilizo na urazini.

Uchaguzi ambao mhusika anahimizwa kufanya na msimulizi ambao ni wa kuvumilia unatawaliwa na kigezo cha furaha. Msimulizi anamtia moyo mhusika kuwa hata kama amepatwa na shida nyingi avumilie kwani hiyo ni hali ya maisha na hakuna mtu asiyepitia hayo. Anamweleza kuwa kila lenye mwanzo lina mwisho ni vile tu mwisho wa matatizo yake haujatimia. Ufikapo, matatizo yake yatakwisha ambapo hayo yakifanyika atafurahi.

Hili linaonyesha kuwa sababu kuu ya kuvumilia ni kuweza kukabiliana na shida anazopitia kwa urazini huku akitarajia kuwa hatimaye zitaisha na hapo ndipo uchungu anaohisi utapungua. Akishindwa kuvumilia basi, atashindwa kukabiliana na matatizo yanayomkumba hivyo atapata madhara zaidi badala ya kuyatatua matatizo hayo kwa uvumilivu. Anayeathiriwa na tendo la kuvumilia katika wimbo huu ni mhusika anayehimizwa kufurahi.

Tendo la kuvumilia kwa hivyo litaleta athari ya kupungua kwa uchungu kwa mhusika. Mhusika anahimizwa kuwa kila kitu huenda kwa utaratibu wake kwa hivyo siku itakapofika ya matatizo yake kufika kikomo ndipo atafurahi. Tendo hili la kuvumilia basi ni tendo lililo adilifu kwani linasababisha kupungua kwa uchungu anaoihisi mhusika kutokana na matatizo yanayomkabili.

Kwa kutumia vigezo vya kuamua iwapo tendo ni adilifu au si adilifu kwa kupima uchungu upunguzwao/ uongezwao na tendo fulani, tendo la kuvumilia lina athari zifuatazo. Katika kigezo cha ukali, uchungu anaohisi mhusika unapungua kwa kiwango cha juu kwani kuvumilia kunamwezesha kusubiri hadi shida zinazomkabili ziishe bila kuathiriwa na shida hizo. Msimulizi anamwambia kuwa "siku ikifika, hata wewe utatambua kwani mambo yote sasa yatakamilika."

Hapo basi ndipo atafurahi. Katika kigezo cha uwezekano, mhusika anapewa matumaini kuwa shida anazopitia zitaisha maanake si za kudumu. Siku yaja ambapo yote hayo yataisha kwa sababu hakuna lisilo na mwisho. Yakiisha, uchungu anaohisi utapungua/ utaisha. Katika kigezo cha kiwango, atakayeathiriwa na tendo la furaha ni mhusika pekee.

Vigezo hivi vinadhihirisha kuwa tendo la kuvumilia linapunguza uchungu kwa mhusika kwa hivyo ni tendo lililo adilifu. Kulingana na dini pia, tendo la kuvumilia ni adilifu maanake dini tofauti zinahimiza watu kuwa wavumilivu. Mwimbaji kwa hivyo anahimiza jamii kuwa na uvumilivu kwani utawawezesha kukabiliana na matatizo mengi ambayo hukumba binadamu kila mara.

### 3.6 SHUKRANI

Shukrani ni tendo la kutambua usaidizi au msaada ambao mtu amepata au anaotarajia kupata. Shukrani humtia motisha anayepokea shukrani kuweza kutenda lile tendo tena. Kwa mfano, kwa mujibu wa Carey (1976), majaribio yaliyofanywa ya kuonyesha athari ya kutoa shukrani yalionyesha kuwa, wateja katika duka la mapambo ya vito walioitwa na kisha kupewa shukrani kwa kununua walidhihirisha ongezeko la asilimia 70 la bidhaa walizonunua. Wale ambao waliitwa tu lakini hawakupewa shukrani kwa kununua walidhihirisha ongezeko la asili mia 30 la bidhaa walizonunua. Hatimaye, wale ambao hawakuitwa wala kupewa shukrani hawakudhihirisha ongezeko lolote la bidhaa walizonunua. Hili ni dhihirisho kuwa, tendo la kushukuru lina manufaa kwa mtenda na mtendwa kwa hivyo bila shaka ni tendo lililo adilifu. Katika mfano huu, linasababisha furaha kwa mteja kiwango cha kumfanya anunue bidhaa zaidi. Hili linasababisha furaha kwa muuzaji maanake atauza bidhaa nyingi hivyo kupata faida kubwa.

Msanii Joseph Ngala anaangazia maudhui ya shukrani katika wimbo unaoitwa *Simba*. Msimulizi anaanza kwa kuonyesha majuto aliyonayo kwa kumsaidia simba kwa sababu baada ya yeye kumsaidia, sasa anataka kumla. Mhusika anamweleza simba afikirie kwa makini maanake alimtoa msituni alikokuwa anaishi kwa taabu lakini sasa ni kama amesahau fadhila zake na anataka kumwangamiza. Anaendelea kusema kuwa simba huyu amekosa shukrani kwa sababu anayomtendea ni sawa na mtu anayeukata mkono unaomlisha. Msimulizi anasema haya katika ubeti wa kwanza ambapo anasema kuwa:

Simba we hatuzoeani, ni heri urudi nyumbani
Nyumbani kwenu ni mwituni, simba fikiria kwa makini
Niliyekuleta mjini, wataka kunila na mimi
Wataka kunila na mimi, simba wewe huna shukrani.

Ubeti huu unaonyesha msimulizi ana uchungu sana moyoni, amechoshwa na simba na ana majuto ya kumtoa mwituni maanake amekosa shukrani. Badala ya kumwonyesha kuwa anamshukuru kwa kumtoa msituni alikotaabika, sasa anataka kumwangamiza.

Msimulizi pia analalamika kuwa alimvalisha mhusika miwani lakini sasa anajifanya hamuoni kuonyesha kuwa alimwerevusha na kumfanya aone mengi kwa mtazamo mpya, tofauti na ilivyokuwa awali. Msimulizi anahisi uchungu kuwa baada ya kumfanyia mhusika hayo sasa anampuuza. Hata hivyo, anamtahadharisha simba kuwa hizo kucha anazotaka kumuumiza nazo atazikata hivi karibuni. Msimulizi anasikitika kuwa akimfukuza maanake amemchosha, ataingia mwitu gani? Haya yanajitokeza katika ubeti wa nne ambapo msimulizi anasema kuwa:

Simba wajifanya kuhani, hata mimi mwanachuoni
Mi nilokuvesha miwani, sasa wajifanya hunioni
Hizo kucha ni za mwituni, tutazikata karibuni
Tutazikata karibuni, simba we huna shukrani.

Mtunzi katika wimbo huu ametumia mhusika simba kupitia mbinu ya sitiari kwani anarejelea mwanamke aliyeolewa na msimulizi ambapo kabla ya kumuoa alikuwa katika hali ya umaskini na taabu nyingi. Vilevile, alikuwa anachezewa tu na wanaume wengine (swara na kongoni) ingawa hakuwa aking’amua hivyo. Msimulizi kwa hivyo alimuonea mhusika huruma sana kwa hivyo akaamua kumuoa ili amnasue kutoka kwa shida nyingi zilizokuwa zinamkabili lakini sasa msimulizi anajuta maanake baada ya fadhila hizi, sasa mwanamke huyu (mhusika) ameyasahau yote hayo na alikotoka na sasa anataka kumwangamiza. Hii ina maana kuwa yawezekana mwanamke huyu anataka kumuua mumewe (msimulizi) ili aweze kurithi mali yake yote. Simba ni mnyama ajulikanaye kwa ukali wake kwa hivyo, mwandishi amemtumia ili kusisitiza matatizo mengi yaliyomkabili hivi kwamba ukali mwingi alionao haungemsaidia katika kumtoa kwenye matatizo yaliyomkabili; lazima angehitaji usaidizi. Mtunzi pia anataka kuonyesha namna simba alivyomgeukia msimulizi baada ya kusaidiwa na kwa ukali kutaka kumwangamiza.

Tunaweza kwa hivyo kulieleza tendo la kutoa shukrani katika misingi ya maadili. Hii ni kwa sababu tendo hili linarejelea mwanamke ambaye alikabiliwa na matatizo mengi lakini badala ya kumshukuru mwanamume aliyemnasua kutoka kwa majanga hayo kwa kumuoa, anamgeuka na kutaka kumwangamiza. Pili, mhusika anayerejelewa kwa mbinu ya sitiari ni mwanamke aliye na uhuru wa kuchagua iwapo amshukuru aliyemsaidia au la. Tatu, mwanamke mhusika ana fikra zilizo na urazini za kumwezesha kufanya uamuzi mwafaka wa kumshukuru aliyemsaidia wala si kumwangamiza.

Tendo hili la mhusika la kukosa shukrani linamwongeza msimulizi uchungu mwingi na majuto. Msimulizi alihisi uchungu kwa kumuona mhusika akiteseka ndipo anaamua kumsaidia lakini badala ya mhusika amshukuru, anapanga kumwangamiza. Hili linamwongezea uchungu aliokuwa nao. Katika ubeti wa pili, msimulizi anamkumbusha simba alikotoka maanake anaona kuwa amesahau. Anamweleza kuwa alimtoa msituni ambamo alichezewa na kudhulumiwa na wanyama wengine kama vile swara na kongoni kiasi cha kumfanya ale majani. Simba ni mnyama alaye nyama lakini msimulizi anaeleza kuwa alimpata akila majani kusisistiza namna alivyokuwa na shida kubwa mwituni ya kukosa chakula hadi ikamlazimu kula majani. Hii ina maana kuwa mwanamke aliyeolewa na msimulizi alikuwa anaishi katika hali duni sana kiasi cha kukosa hata chakula kisha alikuwa akitaniwa tu na wanaume wengine lakini hakuweza kung'amua kuwa wanamtania. Msimulizi kwa hivyo alimuonea huruma sana na kuamua kumuoa ili kumtoa katika hali hiyo ya umaskini. Hata hivyo, msimulizi analalamika kuwa malipo ya kumtoa huko na kumleta kwake anakomtunza vyema ni kutaka kumwangamiza badala ya kumshukuru. Hili linamwongezea msimulizi uchungu mwingi ndiposa anasema kuwa:

Ni malipo kuja mwituni, nilikukuta taabani
Kina swara kina kongoni, wakuchezea na huwaoni
Mwisho waanza kula majani, nikakuonea imani
Nikakuonea imani, sasa yametoka kichwani.

Tendo hili la kukosa shukrani linatosheleza kanuni ya faida kwani linasababisha majuto na uchungu kwa msimulizi kwa hivyo ni tendo lisilo adilifu. Vilevile, tendo hili linamwathiri msimulizi kwani ndiye aliyejitolea kumsaidia mhusika lakini malipo anayopata ni mhusika kumwonyesha ujeuri na kupanga kumwangamiza.

Kwa kutumia vigezo vya kuamua iwapo tendo ni adilifu au si adilifu kwa kupima uchungu upunguzwao/ uongezwao na tendo fulani, tendo la kukosa shukrani katika wimbo wa *Simba* lina athari zifuatazo. Katika kigezo cha ukali wa uchungu, msimulizi anahisi uchungu mwingi maanake alijitolea kumsaidia mhusika ambaye alikuwa taabani sana kiwango cha hata kukosa chakula kifaacho na kutishiwa na wanyama wengine msituni lakini badala ya kumshukuru, anapanga kumwangamiza. Katika kigezo cha muda, msimulizi anasema kuwa imepita miaka saba toka amtoe simba msituni lakini katika kipindi hicho, amejifanya kuwa mjeuri kwa kutaka kumwongoza kwake nyumbani na kupanga kumwangamiza. Hili linaonyesha kuwa amehisi uchungu kwa muda mrefu (miaka saba) ambapo simba aliyemtoa mwituni amekuwa akimwonyesha kiburi badala ya kumshukuru.

Kuna uwezekano kuwa simba akosapo shukrani kwa msimulizi, msimulizi atahisi uchungu. Hii ni kwa sababu msimulizi anatarajia kuwa akimtoa simba mwituni anamokosa chakula na wanyama wengine kumdhulumu, atanyenyekea na kumheshimu lakini badala yake anamwonyesha ujeuri na kupanga kumwangamiza. Katika kigezo cha kiwango, ni msimulizi ambaye anaathiriwa na tendo la mhusika la kukosa kuonyesha shukrani kwake.

Vigezo hivi vinadhihirisha kuwa tendo la kukosa shukrani linasababisha ongezeko la uchungu mwingi kwa msimulizi na kwa muda mrefu kwa hivyo ni tendo lisilo adilifu. Mtunzi kwa hivyo anahimiza jamii kuwa wenye shukrani maanake kutasababisha kupungua kwa uchungu kwa hivyo hili ndilo tendo adilifu.

### 3.7 USHIRIKIANO

Kuungana ni kuweza kuhusiana vyema na wengine. Muungano huleta ushirikiano kwa sababu unapohusiana vyema na wengine utaweza kufanya shughuli tofauti kwa pamoja. Kwa mujibu wa kamusi ya Kiingereza ya Collins (1979), ushirikiano ni kuweza kufanya kazi kwa pamoja na kusaidiana ili kutimiza lengo fulani. Ushirikiano huwezesha watu kufanya mambo ambayo hayawezi yakafanywa na mtu mmoja. Watu wanaposhirikiana, inapaswa kila mtu akubali kufuata sheria ambazo zitawasaidia kufanya kazi kwa pamoja na zitakazomlinda kila mtu na kumfanya kila mtu afurahi. Ili kuweza kushirikiana, mtu anapaswa kuzingatia mahitaji ya wengine kwanza wala si mahitaji yake binafsi. Aidha, ushirikiano huleta watu pamoja na

kuwasaidia kuona usawa baina yao na kuelewa tofauti zao. Husaidia kuepukana na migongano ili kuwa na amani. Ushirikiano ni maadili yanayohitaji kuhimizwa katika jamii kwani huchangia katika kuleta mfumo wa ujamaa na kuondoa ule wa kibepari ambao kila mtu hunuia kujinufaisha bila kujali mwenzake.

Joseph Ngala amezungumzia maadili haya ya ushirikiano katika wimbo unaoitwa *Kisulisuli*. Msimulizi anaeleza hofu yake kuwa anaona kisulisuli kikiwajia kwa ukali na anaona ni hatari kumaanisha kuwa kinaweza kuwaangamiza. Anaeleza kuwa anaona kisulisuli kikiwajia kutokana nao kuwa mbali/ kujitenga na kutoshirikiana. Kisulisuli hapa kimetumika kwa maana ya kizunguzungu ambacho kinapompata mtu huumwa na kichwa na kuanza kuyumbayumba. Msanii ametumia neno hili kwa njia ya sitiari kumaanisha kuwa ni shida kuu ipatayo mtu hata akashindwa kufanya lolote kiasi cha kuyumbayumba. Msimulizi anaeleza kuwa kisulisuli huwapata watu kutokana na wao kutengana/ kukosa kushirikiana katika ubeti wa kwanza anaposema kuwa:

Hiki ni kisulisuli, chenye upepo mkali
Kinakuwa kwetu ni hatari, kila nikikifikiri
Vile tuko mbalimbali, nakionea kisulisuli

Katika ubeti wa pili, msimulizi anawasihi wahusika waache kutengana na badala yake waungane kwani hata Mola mwenyewe hangetaka watengane kuonyesha kuwa ushirikiano ni suala ambalo husisitizwa hata katika dini. Kutoshirikiana basi ni kinyume na atakayo Mungu.

Msimulizi anaeleza kuwa watu wote wanafaa kushirikiana hata kama wana tofauti nyingi kwani la muhimu ni kuwa wote ni binadamu. Hii ndio maana msimulizi katika ubeti wa pili anasema kuwa:

Njoo tushirikiane, kabisa tusitengane
Mola hakupanga, hivyo kamwe
Uwe mwekundu mweusi, na hata uwe mweupe
Lakini damu ni ile ile.

Maelezo katika ubeti huu yanadhihirisha kuwa, tendo la kushirikiana linaweza kuainishwa katika msingi wa maadili kwa sababu linatosheleza vigezo vinavyohitajika kutimizwa ili tendo liweze

kutathminiwa katika msingi wa maadili. Kigezo cha kwanza ni kuwa tendo linafaa kuwa la kibinadamu. Wahusika wanaohimizwa kushirikiana katika wimbo huu ni binadamu ambao wana tofauti mbalimbali kama vile za rangi (uwe mwekundu, mweusi na hata uwe mweupe). Wahusika hawa wanatarajiwa kuwa na maadili ya ushirikiano. Katika kigezo cha uhuru, wahusika katika wimbo huu wana uhuru wa kutoshirikiana au kushirikiana na msimulizi ili waweze kukabiliana na matatizo ambayo msimulizi anaona yatawashinda iwapo hawatashirikiana. Kigezo cha mwisho ni fikra zilizo na urazini. Inadhihirika katika wimbo huu kuwa wahusika wana ufahamu ulio kamili unaofaa kuwawezesha kutathmini athari ya kushirikiana na kutoshirikiana hivyo kufanya uamuzi ulio mwafaka.

Kigezo kikuu kinachomfanya msimulizi kuwahimiza wahusika washirikiane naye ni furaha. Msimulizi anawahimiza wahusika washirikiane naye maanake anaona shida kuu (kisulisuli) ikiwajia kwa mbali. Katika ubeti wa kwanza, msimulizi anasema kuwa anakiona kisulisuli kikiwajia kwa ukali ambao ni hatari na kutokana na umbali walio nao, anahofia kuwa shida hii itawaangamiza. Hili linajitokeza katika ubeti wa tatu ambapo msimulizi anaeleza kuwa:

Tuliyonayo ni safari, na mbele ni kisulisuli
Cha mabonde hata majabali, kuna upepo mkali
Wavuma kila mahali, kutuletea kisulisuli x2

Katika ubeti huu msimulizi anaeleza kuwa wako katika safari ndefu ambayo imejaa changamoto nyingi. Anaeleza kuwa shida iliyo mbele yao ni ya kutamausha kwa hivyo wasiposhirikiana, hawataweza kuikabili shida hiyo, jambo litakalowaletea majonzi. Maelezo haya yanaonyesha kuwa msimulizi anawahimiza washirikiane ili waweze kukabiliana na tatizo lililo mbele yao (kisulisuli), jambo litakalowapunguzia uchungu.

Waathiriwa wa tendo hili ni msimulizi na wahusika. Msimulizi anawahimiza wahusika washirikiane naye ili kuweza kukabiliana na matatizo anayoona yatawashinda iwapo hawatashirikiana. Anasema kuwa wakishirikiana, watakiweza kisulisuli (shida), jambo litakalowapunguzia uchungu lakini wasiposhirikiana watawezwa na kisulisuli kitakachowaumiza kichwa na kuwafanya wawe na huzuni.

Kwa kutumia vigezo vya kuamua iwapo tendo ni adilifu au si adilifu kwa kupima uchungu upunguzwao/ uongezwao na tendo fulani, tendo la kushirikiana linaleta athari mbalimbali. Kwa

kutumia kigezo cha ukali wa furaha uletwao na tendo, tendo la kushirikiana linatoa furaha kuu kwa wahusika. Msimulizi anaeleza kuwa wahusika wakishirikiana naye wataweza kukabiliana na matatizo mengi yaliyo mbele yao, jambo litakalowapunguzia uchungu wa kukabiliwa na matatizo hayo. Katika kigezo cha uwezekano, kuna uwezekano mkubwa kuwa wahusika wakishirikiana na msimulizi wataweza kukabiliana na matatizo yaliyo mbele yao. Msimulizi anasema kuwa anakiona kisulisuli kikiwajia kwa ukali hasa kwa vile wako mbali lakini wakiungana watakiweza kisulisuli hiki. Katika kigezo cha kiwango, wanaoathiriwa na tendo hili ni msimulizi pamoja na wahusika wanaohimizwa kushirikiana.

Vigezo hivi vinadhihirisha kuwa ushirikiano husaidia watu kukabiliana na matatizo mengi yanayowakabili katika maisha, jambo ambalo huwaepusha kupata uchungu wa athari ya matatizo hayo kwa hivyo ni tendo lililo adilifu. Joseph Ngala kwa hivyo anawahimiza wanajamii kushirikiana licha ya tofauti mbalimbali walizonazo kwani, ushirikiano utaweza kutatua shida ambazo ni ngumu kutatuliwa na mtu mmoja.

### 3.8 UWAJIBIKAJI

Uwajibikaji ni mojawapo ya maadili muhimu katika jamii. Kwa mujibu wa kamusi ya Kiingereza ya Collins (1979*)*, kuwajibika ni kuweza kuchukua wajibu wa tendo fulani au kwa mtu fulani. Neno hili pia lina maana ya kitendo cha mtu mwenye wadhifa kuchukua dhamana ya kosa lililofanywa ama na yeye au mtu mwingine aliye chini yake. Katika utafiti wetu, tumetumia maana ya kwanza ya kuwajibika. Neno hili hutumiwa kila mara tunapozungumzia kwa mfano kiongozi/ msimamizi aliyewajibika, mashirika yaliyo na uwajibikaji wa kijamii, mzazi aliyewajibika n.k. Hapa, neno uwajibikaji linatumika kama sifa ya mtu kuonyesha kuwa, kama mtu amewajibika basi ni mwadilifu na kama hawajibiki, si mwadilifu.

Mtu aliyewajibika anaweza kutegemewa katika kufanya maamuzi na kutenda matendo mbalimbali kwa njia iliyo adilifu. Kwa kuzingatia kigezo cha majukumu apewayo mtu, mtu aliyewajibika ni yule anayeweza kuaminiwa katika kuanzisha/ kuvumbua jambo na anaweza kuchukulia majukumu yake kwa makini. Pia anaweza akakubali kuwa amekosea iwapo wajibu anaopaswa kutekeleza ameutekeleza kwa njia iliyo na dosari. Vilevile, mtu aliyewajibika hutumika kama kielelezo cha uadilifu, hutathmini matendo yake ya awali kwa makini hivi

kwamba hukubali iwapo amekosea kisha huchukulia majukumu apewayo kwa makini kwa kuwaza anafaa kutenda nini na vipi ili atende kwa njia ifaayo. Mtu asiyewajibika ni yule asiyechukulia wajibu wake kwa makini.

Joseph Ngala anaangazia maudhui ya uwajibikaji katika wimbo uitwao *Jembe*. Wimbo huu unaeleza kuwa mhusika alimpa mwanawe anayeitwa Jembe shamba lililo na rutuba na mimea mingi ili alilime. Hata hivyo, jambo linalomshangaza mhusika na kumpa majonzi ni kuwa mwanawe (Jembe) alikimbia na kuliacha shamba hilo. Msimulizi ametumia jina Jembe kuonyesha kuwa mtoto aliyepewa kazi ya kulima shamba lenye rutuba alikuwa na uwezo wa kufanya hivyo maanake jembe ni kifaa kitumiwacho kulima. Hata hivyo, mtoto huyu amekosa kuwajibika kwa kukataa kabisa kulilima shamba, jambo linalomkera mzazi wake. Haya yanadhihirika katika ubeti wa kwanza ambapo msimulizi anasema kuwa:

Alosema kwenye, vikoko hakuna wajenzi
Alisema kweli, hata nami nampa pongezi
Ninaye mwanangu, kwa jina yuaitwa Jembe
Jembe mwana huyu, kwa kweli sijamuelewa
Nilimpa shamba, apate kulipalilia
Shamba la rutuba, tena kwa wingi wa mimea
Siku za dhoruba, nipate kumsaidia
Sina nijualo kumbe, shamba kalikimbia.

Mhusika anaendelea kueleza majuto yake katika ubeti wa pili kwani, baada ya Jembe kuliacha shamba, sasa linachezewa na nyani na tumbili. Badala ya mwanawe (Jembe) kulilima shamba ili wapate chakula maanake lina rutuba, mwanawe analiacha liharibiwe wanyama. Haya yanamghadhibisha sana mzaziwe na kumfanya ajute kwa kumpa jukumu la kulilima shamba hilo. Mhusika anajaribu kumsihi mwanawe arudi shambani lakini anakataa.

Mtunzi katika wimbo huu ametumia mbinu ya sitiari kwa kutumia jina Jembe kurejelea mwanawe kisha shamba kurejelea msichana ambaye msimulizi alimuoza mwanawe Jembe. Msimulizi anasema kuwa alimuoza msichana huyu kwa mwanawe maanake ni msichana mrembo (mate yadondoka, shamba zuri kama halua) kisha mwenye uwezo wa kuwa mke mzuri

wa kumfaa (shamba la rutuba, tena kwa wingi wa mimea). Hata hivyo, msimulizi anajuta maanake mwanawe alimtoroka msichana huyu bila kujali na kumuachia wanaume wengine wamchezee (matumbili na manyani). Hili linamghadhibisha sana msimulizi.

Utangulizi huu unaonyesha kuwa, tendo hili la kuwajibika linaweza likachanganuliwa kwa msingi wa maadili. Hii ni kwa sababu kwanza, mhusika anayerejelewa katika wimbo huu ni binadamu (mwanawe msimulizi) ingawa mwimbaji ametumia mbinu ya sitiari kwa kutumia jina Jembe. Mhusika huyu ni kiumbe anayetarajiwa kuchukulia wajibu anaopewa wa kumtunza mkewe kwa makini maanake ana uwezo wa kufanya hivyo ingawa anaamua kumtoroka. Pili, ana uhuru wa kuchagua amtunze mkewe au la. Anapewa msichana mchanga na mrembo amtunze lakini anachagua kumtoroka. Tatu, ana ufahamu ulio kamili ambao tunatarajia utamwezesha kufanya uamuzi kwa urazini wa kumtunza mkewe lakini anafanya kinyume kwa kumtoroka na kumwachia wanaume wengine wawe na uhusiano naye.

Kigezo kinachomsukuma msimulizi kumpa mtotowe shamba (msichana) ili kulipalilia (kumuoa na kumtunza) ni furaha. Msimulizi anamtafutia mtotowe msichana mchanga na mrembo ili kumuoa apate kuishi maisha mema naye. Hata hivyo, anahuzunika maanake mtotowe amemkimbia msichana huyu mrembo na kumuacha achezewe na wanaume wengine. Msimulizi alitarajia kuwa mtotowe atamtunza na kuishi naye ili wapate kufanikiwa maishani. Anaona kuwa kama angefanya hivyo, wangefurahi sana kwani wangeiletea familia yake ufanisi. Hii ndio maana anasema kwa kutumia sitiari kuwa anahuzunika na kulimezea shamba hilo mate kwani limeachiwa wanyama kuliharibu ilhali lina rutuba.

Iwapo mhusika angewajibika kwa kulilima shamba kama anavyotarajia mzaziwe, jambo hilo lingempunguzia uchungu msimulizi kwani anauchungu wa kumwona mwanawe akiwa kapera. Vilevile, hangepata uchungu wa kuliona shamba hilo likiharibiwa na wanyama kama vile tumbili. Hii ina maana kuwa kama mhusika angemtunza mkewe vyema wangefanikiwa sana maishani; si kwa mali tu bali pia msimulizi angefurahi kwa kuzaliwa wajukuu. Hili linaonyesha kuwa athari ya tendo la kuwajibika ni kupunguza uchungu. Anayeathiriwa na tendo hili la kutowajibika ni msimulizi kwani ndiye analalamika kuhusu uchungu mwingi anaohisi kutokana na mtotowe kukosa kumtunza mkewe na kumuacha achezewe na wanaume wengine.

Kwa kutumia vigezo vya kuamua iwapo tendo ni adilifu au si adilifu kwa kupima uchungu upunguzwao/ uongezwao na tendo fulani, tendo la kuwajibika lina athari mbalimbali. Katika kigezo cha ukali, msimulizi anapata ongezeko la uchungu mwingi unaotokana na mhusika kukosa kuwajibika na kumuacha mkewe aliye mrembo sana achezewe na wanaume wengine. Muda ambao mhusika amehisi uchungu huu si mrefu maanake haidhihiriki kuwa ni muda mrefu umepita toka mtotowe amuache mkewe.

Kwa kuangazia kigezo cha uwezekano, kuna uwezekano kuwa mhusika akimuacha mkewe, msimulizi atahisi uchungu zaidi. Hii ni kwa sababu msimulizi anasema kuwa anampa mtotowe mke mzuri, uzuri anaoulinganisha na halua maanake aliona kuwa mtotowe ana uwezo wa kumtunza. Anatarajia kuwa mhusika atachukua jukumu la kumtunza mkewe ili wapate kufanikiwa kwa pamoja maishani kwa hivyo akitenda kinyume basi kuna uwezekano kuwa msimulizi atahisi uchungu mwingi. Katika kigezo cha kiwango, anayeathiriwa na tendo hili la kukosa kuwajibika ni msimulizi.

Mtunzi kwa hivyo anakashifu tendo la kutowajibika ambalo hutokea katika jamii kwa watu ambao hupewa majukumu mbalimbali lakini wanakataa kuyatilia maanani/ kuyatekeleza ingawa wana uwezo wa kuyatekeleza. Tendo hili si adilifu maanake huongeza uchungu na masikitiko kwa wanaohusika kama alivyohisi mhusika. Mtunzi kwa hivyo anawahimiza wanajamii kuwa wenye uwajibikaji maanake wakifanya hivyo, watasababisha kupungua kwa uchungu kwa hivyo tendo la kuwajibika ndilo tendo adilifu.

### 3.9 HITIMISHO

Katika sura hii, tumechanganua maudhui ya uadilifu yanayojitokeza katika nyimbo tulizoteua tisa za Joseph Ngala ambazo ni *Fuateni mambo ya sheria*, *Mwana Mpotevu, Ndivyo Ilivyo dunia*, *Nisikilize Mwanangu, Ndugu Tupendane, Dada Vumilia*, *Simba, Kisulisuli na Jembe.* Katika nyimbo hizi, maudhui ya uadilifu ambayo yamejitokeza ni pamoja na kutii sheria, kutokuwa na tamaa, kusikiliza mawaidha kutoka kwa wakuu, upendo uvumilivu, shukrani, ushirikiano na uwajibikaji. Tumeyabainisha maudhui haya katika nyimbo hizo na kuonyesha kama yanafaa kuainishwa kama ni adilifu au si adilifu na ni vipi ni adilifu kwa kutumia nadharia ya unufaishaji hasi. Pia tumeonyesha matendo haya yanatoa athari gani kwa walengwa ambao ni mtu binafsi au jamii.

# SURA YA NNE

# HITIMISHO

## 4.0 UTANGULIZI

Sura hii inalenga kuangazia muhtasari wa matokeo yetu ya utafiti. Kutokana na matokeo yetu ya utafiti, tumeweza kujadili maswali yaliyoongoza utafiti wetu pamoja na malengo ya utafiti. Vilevile tumeangazia changamoto tulizokumbana nazo katika utafiti wetu pamoja na mapendekezo.

## 4.1 MUHTASARI WA UTAFITI

Utafiti ambao tumefanya ulidhamiria kuchunguza maudhui ya uadilifu katika nyimbo tisa tulizoteua za Joseph Ngala ambazo ni *Fuateni Mambo ya Sheria, Mwana Mpotevu, Ndivyo ilivyo Dunia, Nisikilize Mwanangu, Ndugu Tupendane, Dada Vumilia, Simba, Kisulisuli, na Jembe.* Malengo yetu ya utafiti yalikuwa matatu ambayo ni:

iv. Kuchanganua maudhui ya uadilifu katika nyimbo za Joseph Ngala.
v. Kuonyesha faida / athari ya maadili katika jamii.
vi. Kuonyesha sababu thabiti ya kuwa tendo ni adilifu.

Vilevile, utafiti huu ulikusudia kujibu maswali yafuatayo:

iv. Je, ni matendo yepi adilifu yanayojitokeza katika nyimbo tulizoteua za Joseph Ngala?
v. Je, matendo hayo adilifu yanatoa athari zipi kwa walengwa (jamii/ mtu binafsi)?
vi. Je, kunayo sababu thabiti ya kuainisha matendo hayo kama adilifu?

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya unufaishaji hasi ya Popper (1945). Nadharia hii ilitusaidia kuchanganua maudhui ya uadilifu katika nyimbo tulizoteua za Joseph Ngala. Nadharia hii pia imetusaidia kueleza ni vipi matendo yanayojitokeza katika nyimbo hizi ni adilifu hasa kwa kuonyesha kama yanapunguza au kuongeza uchungu kwa walengwa, athari ya tendo husika kwa jamii au mtu binafsi na kielelezo cha kupima uchungu uongezwao/ upunguzwao na tendo husika.

Kazi hii imewasilishwa katika sura tatu ambapo uwasilishaji huu umefanywa kwa njia ya maelezo yaliyoandikwa. Sura ya kwanza imejumuisha vipengele muhimu vilivyoongoza utafiti wetu ambavyo ni kama vile usuli wa mada, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada tuliyoshughulikia, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada tuliyoshughulikia, msingi wa nadharia na hatimaye, mbinu tulizotumia za utafiti. Sura hii ilikuwa kama dira ya utafiti wetu.

Katika sura ya pili, tuliangazia historia fupi ya Joseph Ngala, asili ya mtindo wa nyimbo za bango, maelezo ya dhana ya uadilifu na ya nyimbo. Haya yalitoa mwanga kuhusiana na suala tuliloangazia la maudhui ya uadilifu katika nyimbo za bango za Joseph Ngala. Vilevile tulieleza nyimbo za Joseph Ngala ni za aina gani kulingana na aina tofauti za nyimbo ambazo tulielezea.

Sura ya tatu iliangazia maudhui ya uadilifu ambayo Joseph Ngala ameyazungumzia katika baadhi ya nyimbo zake ambazo ni *Fuateni Mambo ya Sheria, Mwana Mpotevu, Ndivyo ilivyo Dunia, Nisikilize Mwanangu, Ndugu Tupendane, Dada Vumilia, Simba, Kisulisuli na Jembe*.. Maudhui haya ni kutii sheria, kutokuwa na tamaa, kusikiliza mawaidha kutoka kwa wakuu, upendo, uvumilivu, shukrani, ushirikiano na uwajibikaji. Tulichanganua maudhui haya kwa kutumia mihimili ya nadharia ya unufaishaji hasi pamoja na vigezo vya kupima uchungu uongezwao/ upunguzwao na tendo husika. Aidha, tulifafanua masuala muhimu ya matendo tuliyochambua kama vile sheria, dini na utamaduni na jinsi yanavyohusiana na tendo husika na kutoa sababu thabiti ya kueleza tendo husika kama adilifu. Maadili haya ni muhimu katika kuleta utangamano katika jamii yoyote ile.

## 4.2 MUHTASARI WA MATOKEO

Utafiti tuliofanya ulipata matokeo yafuatao kulingana na maswali ya utafiti yaliyotuongoza. Kwanza, utafiti huu ulidhihirisha kuwa nyimbo tisa tulizoteua za Joseph Ngala zina maudhui ya uadilifu. Maudhui haya yaliyojitokeza katika nyimbo hizi ni pamoja na kutii sheria, kutokuwa na tamaa, kusikiliza mawaidha kutoka kwa wakuu, upendo, uvumilivu, shukrani, ushirikiano na uwajibikaji.

Pili, utafiti huu ulibainisha kuwa kutenda matendo haya adilifu kunapunguza uchungu anaohisi mtu binafsi au jamii lakini kutenda kinyume chake kunasababisha ongezeko la uchungu. Kwa mfano, katika wimbo wa *Fuateni Mambo ya Sheria*, kutokana na mhusika kutofuata sheria ya

kutoiba, anafungwa gerezani akiwa bado kijana jambo linalosababisha ujana wake kuishia gerezani. Anafungwa kwa miaka saba na kazi ngumu gerezani hivyo anapata ongezeko la uchungu aliokuwa nao kwa kukosa pesa. Watu wanaoibiwa pia vilevile wanapata uchungu kwani wanakerwa sana na tendo la mhusika kuwaibia. Athari hizi hasi ndizo zinalifanya tendo hili la kuiba kuwa lisilo adilifu. Sheria na dini pia inakataza tendo hili hivyo kulifanya lisiwe adilifu.

Katika wimbo uo huo, tulieleza kuwa mhusika anatekeleza tendo la kuiba kutokana na tamaa aliyonayo ya kupata pesa kwa haraka. Tamaa hii inamfanya ashiriki katika wizi, tendo linalosababisha ongezeko la uchungu mwingi kwake na jamii husika kama vile tulivyoeleza katika aya iliyo hapa juu. Hili linalifanya tendo hili kutokuwa adilifu. Vilevile tulieleza tendo la kuwa na tamaa ya raha za dunia katika wimbo wa *Mwana Mpotevu*. Mhusika katika wimbo huu alitoroka nyumbani ili kula raha bila kuingiliwa na wazazi wake lakini badala ya kupata raha aliyotarajia, anapata dhiki sana inayomfanya arejee nyumbani. Wazazi wake nao wanahuzunika sana kutokana na mhusika kutoroka kwani hawakufahamu kama ameaga dunia au la, jambo linalowapa huzuni tele. Ongezeko hili la huzuni kwa mhusika na wazazi zinalifanya tendo hili la kuwa na tamaa ya raha za dunia kutokuwa adilifu.

Katika wimbo wa *Ndivyo ilivyo Dunia* na *Nisikilize Mwanangu*, maudhui ya kusikiliza ushauri wa wakuu yalijitokeza. Katika wimbo wa kwanza, mhusika alijuhusisha na urafiki na mpenziwe licha ya kukanywa na wazazi wake. Hatimaye mpenziwe anamuacha na ndipo akagundua kuwa alikuwa tu anamhadaa. Haya yalimtia uchungu sana na majuto ya kutosikiliza ushauri wa mzazi wake hivyo kulifanya tendo hili kuwa si adilifu. Katika wimbo wa pili, msimulizi anamuonya mhusika kuwa kutosikiliza mawaidha ya wazazi na kufanya kinyume na wanayomshauri kutamfanya apate laana kutoka kwa Mungu. Vilevile, mzaziwe anapata huzuni zaidi kutokana na mtotowe kupuuza anayomshauri. Athari hizi hasi zinalifanya tendo hili kutokuwa adilifu.

Katika wimbo wa *Ndugu Tupendane*, tulieleza maudhui ya uadilifu ya upendo. Tulibaini kuwa msimulizi anawashauri wahusika wapendane na waepukane na kutengana. Wakifanya hivyo, wataweza kukabiliana na tatizo lolote litakalowakabili na kwa haraka. Jambo hili anaeleza kuwa litawapa baraka na kupunguza uchungu ambao wangehisi iwapo wangekabiliwa na matatizo kutokana na kutengana. Matokeo haya chanya yanalifanya tendo hili la kupendana kuwa adilifu.

Katika utafiti wetu, vilevile tulieleza maudhui ya uvumilivu yanayojitokeza katika wimbo wa *Dada Vumilia*. Mhusika katika wimbo huu anahimizwa avumilie licha ya matatizo mengi yanayomkabili. Anahimizwa kuvumilia kwani dunia ina mazuri na pia mabaya kwa hivyo akikumbwa na mabaya, si ya kudumu bali yataisha. Hata hivyo, akishindwa kuvumilia atatamauka na kupata madhara. Uvumilivu hata hivyo utamwezesha kusubiri hadi matatizo yanayomkabili yaishe, jambo litakalomsaidia kupunguza uchungu anaohisi. Tulibaini kuwa kigezo cha kupungua kwa huzuni/ uchungu atakayopata mhusika baada ya matatizo kuisha ndicho kinalifanya tendo la uvumilivu kuwa adilifu.

Katika wimbo wa *Simba*, tulieleza maudhui ya shukrani. Katika wimbo huu, msimulizi anapata uchungu mwingi na majuto kutokana na fadhila alizomtendea mhusika kwa kumwokoa kutokana na shida nyingi za umaskini zilizokuwa zinamkabili lakini badala ya kumshukuru, alimgeuka na kutaka kumwangamiza. Tendo la kukosa shukrani kwa hivyo si adilifu maanake linampa msimulizi huzuni zaidi.

Maudhui ya ushirikiano nayo yalijitokeza katika wimbo wa *Kisulisuli*. Msimulizi katika wimbo huu anawahimiza wahusika washirikiane ili waweze kukabiliana na shida tele anazoona zitawakabili katika safari yao ya maisha. Anaeleza kuwa shida hizi ni kali na wakishindwa kushirikiana, zitawashinda na kuwaletea maangamizo (kisulisuli). Ushirikiano kwa hivyo utawapunguzia uchungu ambao wangehisi iwapo wangekabiliwa na matatizo hayo hivyo ushirikiano ni sifa adilifu.

Hatimaye katika wimbo *Jembe*, tulieleza maudhui ya uwajibikaji. Katika wimbo huu, msimulizi anamtafutia mwanawe mke mrembo na mchanga wa kuoa lakini mwanawe anamtoroka msichana huyu na kumuachia wanaume wengine wamchezee. Msimulizi alifikiri kuwa mwanawe akipata mke, atamsaidia kufanikiwa maishani na pia msimulizi ataweza kupata wajukuu. Hata hivyo, mwanawe anakosa kuwajibika na kumtoroka msichana huyu, jambo linalompa msimulizi uchungu zaidi. Kutokana na athari hizi anazopata msimulizi, tendo la kutowajibika si adilifu hivyo mwimbaji anawahimiza wanajamii wawe na uwajibikaji kwani ndilo tendo adilifu.

Aidha, tulieleza iwapo matendo katika nyimbo tulizotumia yanafaa kuainishwa kwa msingi wa maadili kisha tukaeleza sababu thabiti za kuainisha matendo hayo kama adilifu kwa kutumia nadharia ya unufaishaji hasi. Katika nadharia hii, tulitumia kanuni ya faida na kielelezo cha kupima kiasi cha uchungu upunguzwao/ uongezwao na tendo husika. Vilevile tulitumia msingi wa dini na sheria ambao pia hutumiwa kuamua iwapo tendo ni adilifu au si adilifu.

## 4.3 CHANGAMOTO ZA UTAFITI

Utafiti wetu ulikumbwa na matatizo kadhaa. Tatizo kuu lililotupata ni kuwa diski za nyimbo zilikuwa nyingi hivyo ilitulazimu kuchukua muda mrefu kuzisikiliza na kuchuja zile zilizofaa kwa kazi yetu kisha kuzinakili. Aidha, muda wa utafiti ulikuwa mfupi hivyo hatukuweza kupata habari zote zilizotakikana. Hata hivyo, licha ya changamoto hizo, tuliweza kukusanya data zilizotufaa katika utafiti wetu.

## 4.4 MAPENDEKEZO

Utafiti wetu ulishughulikia maudhui ya uadilifu katika nyimbo tisa tulizoteua za Joseph Ngala. Tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusu mbinu za lugha alizotumia msanii huyu katika nyimbo zake.

## MAREJELEO


Amonde, O. L. (2006) *Form and Content in Children's Play Songs: A case study of Nairobi province*. (Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi)

Bentham, J. (1789). *Introduction to the principles of Morals and Legislation:* http://www.utilitarianism.com/jeremy-bentham/

Bible Society of Kenya. (1976). *Good News Bible*. Britain: The Bible societies/ Collins.

Bourke, V. J. (1968). *History of Ethics*. New York: Doubleday & Company, Inc.

Bukenya, A. et al. (1994). *Understanding Oral Literature*. Nairobi: Oxford University Press.

Carey, J. R. na wengine (1976). A Test of Positive Reinforcement of Customers. Journal of Marketing, 40.

Collins (1979). *Collins English Dictionary*. Great Britain: Harpercollins Publishers.

Collins (1991) *Collins Dictionary of Sociology*. Great Britain: Harpercollins Publishers.

Dobeljuh, P. (2006). *Ethics: Learning to Live*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

Garrath, W. *Internet Encyclopedia of Philosophy:* http://www.iep.utm.edu/responsi. ISSN 2161-0002.

Gensler, H. J. (1998): *Ethics*. London: T.J Internationa Ltd.

Hobhous, L.T. (1922). *The Elements of Social Justice*. London: George Allen & Unwin Ltd.

Kasau, M. E. (2013). *Maudhui na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Injili za Rose Muhando*. (Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta)

Kieli, M. (1988). *Social critique among the Kamba*. (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Mahugu, P. W. (1990). *A Literature Investigation into the Agikuyu Songs of Independence* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Mjomba, W. G. (2012). *Suala la upole katika nyimbo za harusi kutoka jamii ya Wadawida* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Mugenda na Mugenda (1999). *Research Methods: Quantitave and Qualitative Approaches.* Nairobi: Act Press.

Ngugi, P. M. (2000). *Nafasi ya Muziki uliopendwa katika Fasihi ya Kiswahili.* AAP 64. Swahili Forum VII.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi:* Jomo Kenyatta Foundation.

Owino, M. (2011). *Uchanganuzi wa Matini Teule ya Nyimbo za Foustin Munishi*. (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Rae, B. S. (1973): *Moral Choices*: *An Introduction to Ethics*. USA: International Bible Permission of Zondervan.

Ruggiero, V. R. (2012): *Thinking Critically about Ethical Issues*. USA: MCGraw- Hill companies, Inc.

Sayyid, A. (1939): *Al-Inkishafi: The soul Awakening*. London: Sheldon Press.

Sinha, J. (1978): *A Manual of Ethics*. London: New Central Book Agency (P) Ltd.

Theodores, D. na wengine (2002): *Great Traditions in Ethics*. USA: Eve Howard.

Thompson, M. (1999). *Ethical Theory*. London: Hodder Murray.

Timammy, R. (2002). *Mombasa Swahili Women's Wedding Songs: A Stylistic Analysis* (Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi).

TUKI. (2000). *English-Swahili Dictionary.* Second Edition. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

## KIAMBATISHO

### 1. FUATENI MAMBO YA SHERIA

1. Jama fuateni mambo ya sheria

   Usipofuata utapata taabu sana

   Kama fulani anunua mali ya wizi

   Baada ya saa namkuta kifungoni.

   Ooh mama nasikitika

   Kijana mwema kama huyu jamani katupwa gerezani

   Kwa tamaa ya faida ya wizi

   Ooh mama nasikitika x2

2. Siku ya kesi watu wengi walifika

   Kusikiliza hiyo hukumu yake

   Miaka saba kazi ngumu gerezani

   Ujana wake waishia kifungoni

   Ooh mama nasikitika

   Kijana mwema kama huyu jamani katupwa gerezani

   Kwa tamaa ya faida ya wizi

   Ooh mama nasikitika x2

3. Mali ya wizi wala haina baraka

   ni kama vile mali nyingi ya urithi

   Pata kwa jasho usitafute kwa urahisi

   Vunja mawe utafute kilimo

**2. MWANA MPOTEVU**

1. Wamuona aingia, huyo mwana mpotevu

   Ametanga na dunia, leo amerudi

   Wazazi wamngojea, furaha tele leo

   Amepigwa na dunia, pole mpeni

   Kufika tu mlangoni, yuanza kulia

   Kwa machozi ya usoni, sijui kwa nini

   Baba akamuuliza, mwanangu watoka wapi

   Nieleze nisikie, nipate jua x2

2. Baba mie sistahili, kuitwa tena mwanao

   Ni heri niwe kama, mtumishi wako

   Nimekosa mbinguni, na hata duniani

   Nakuomba kwa hisani, unikubali x2

3. Akamshika mkono, kumpeleka za nyumbani
Nguo zimemchanika, raha za dunia
Baba kamwe hakujali, alimkumbatia
Na kisha akamwambia, kwangu ni kwako
Mwanangu usihuzunike, hii ni nyumba yako
Leo utakula nami, mwanangu sikia
Nakufanyia karamu, na ng'ombe nikuchinjie
Ili upate ujue, kwangu ni kwako.

**3. NDIVYO ILIVYO DUNIA**

1. Nitakapokudokeza, mwenzangu ukanipuuza
Hivi sasa, walia itafaa nini
Ndivyo ilivyo dunia, kua uone mengi.

2. Hali yangu maskini, roho yangu ni tajiri
Nilichopata mwenzangu, tulikula sote
Nikiingia ufinyaji, sikukunyima kamwe.

3. Nilijua akudanganya, nikajaribu kukukanya
Huwezi kunilaumu, kwa yalokupata
Na laiti ungelijua, ungefuata yangu.

4. Hivi umekwama, wabaki kushika tama

Ijapokuwa nakwambia, nakuhurumia

Ndivyo ilivyo dunia, ukae ukijua.

5. Uliyachukua siri, hivi leo yako dhahiri

Asosikia la mkuu, huvunjika guu

Langu ni kukupa pole, ilivyo dunia.

Inua macho yako sasa, cheza na wenzako chakachaka

Kama ni yeye amekuacha, amekimbia utampata } x3

Inua macho yako sasa, cheza na wenzako chakachaka

Inua macho yako sasa } x2

**4. NISIKILIZE MWANANGU**

1. Ewe kijana, hivi sasa wakua

   Watoka mbali, mzigo hujautua

   Pia wendapo mwanangu, bado hujakujua

   Nisikize basi, machache ntakwambia

   Huko uendako, ndiko kwenye dunia

   Pepo zavuma, na jua hata mvua

Na ukifurahi leo, lazima kuelewa
Vimbele vyakungojea.

2. Sote twajua, tuko kama maua
Piga kifua, kesho waanza fifia
Nakisha wafikiria, laiti ungejua
Heri ungejua, sori umeshachelewa
Washika tama, hapo huna la kufanya
Siku za raha, ndio hazirudi tena
Na hata hivi nasema, kisha wanisikia
Najua najisumbua.

3. Macho mawili, ye Mungu hakukunyima
Waona mbali, mbali hata kunishinda
Haki unayo akili, si kwamba uko nyuma
Ni vile hujali, bure wajidanganya
Jaribu sana, upambane na dunia
Bado kijana, bado hujachelewa
Wala usikate tamaa, yote ni majaliwa
Nisikilize mwanangu.

4. Mzazi yule, ndiye aliyekulea

   Imani yake, lake lishamwondokea

   Bali kwa vituko vyako, lawama za dunia

   Akifikiria, mara yuanza kulia

   Machozi yale, yatakapomdondoka

   Utaanguka, na mengi yatakufika

   Na wengi watakusema, huku wasikitika

   Nisikilize mwanangu.

5. Eva ewe Eva wewe, mwenye ngurumo za simba

   Zetu sisi ni za ninga, waimbia wa dunia

   Kila jambo lina mwisho, liwe kubwa liwe dogo

   Hata lije na vitisho, vya wafurahisha macho

   Ni yaivayo, kwao huwa kama sumu

   Wengine wao, huanza kunilaumu

   Ati najifanya chuo, nahubiri wazimu

   Hata mimi ninayo, mbona nawahukumu

   Kijana cheka, uzidi kufikiria

   Mi sina shaka, na mengi nishakwambia

   Nainua mikono juu, umo kwa mola wangu

   Nisikiliza mwanangu x2

Nainua mikono juu, umo kwa mola wangu
Nisikiliza mwanangu } x2

**5. NDUGU TUPENDANE**

1. Kaka dada zangu, hii ni siku nzuri

   Kupata nafasi, ya kuwaelezea

   Hakuna jambo zuri, kama ndugu kupendana

   Kumbukeni utotoni, tukiwa pamoja

   Mola hupanga lake, kila mmoja akawa kwake

   Na ni lazima sote, tujuliane hali

   Kuna hili na lile, pale familia nzuri

   Kuwa na maelewano, huleta baraka kote

2. Kweli ndugu kwa nini hatuelewani?

   Ndugu hukosana, mwisho wakapatana

   Tusiskize, waja kutupotosha

   Wanavyosema, huwa hivi na vile

   Heshima ya wapwani, huwa maelewano

   Mkubwa na mdogo, tuzidi kupendana

   Ewe mola, zidi kutuongoza

   Kwa imani yako, tuzidi kupendana

3. Jama ndugu tupendane, hakuna hili na lile

   Asemaye na aseme, kwani tu pamoja

   Jamaa ndugu tupendane, hakuna hili na lile

   Jambo hili ni muhimu, kwa dhiki na raha x3

Jambo hili ni muhimu, kwa dhiki na raha x2

**6. SIMBA**

1. Simba we hatuzoeani, ni heri urudi nyumbani

   Nyumbani kwenu ni mwituni, simba fikiria kwa makini

   Lililokuleta mjini, wataka kunila na mimi

   Wataka kunila na mimi, simba wewe huna shukrani.

2. Ni malipo kuja mwituni, nilikukuta taabani

   Kina swara kina kongoni, wakuchezea na huwaoni

   Mwisho waanza kula majani, nikakuonea imani

   Nikakuonea imani, sasa yametoka kichwani.

Simba una nini kichwani, hujasahau ya mwituni

Na ukinila hata mimi, utaingia mwitu gani } x2

3. Simba niseme lugha gani, sasa yapata miaka kumi

Bado wanguruma kwa nani, hadi mwituni huna thamani

Umeshanitoka maanani, sijui nikufanye nini

Sijui nikufanye nini, simba we huna shukrani.

4. Simba wajifanya kuhani, hata mimi mwanachuoni

Mi nilokuvesha miwani, sasa wajifanya hunioni

Hizo kucha ni za mwituni, tutazikata karibuni

Tutazikata karibuni, simba we huna shukrani.

**7. DADA VUMILIA**

1. Hebu dada vumilia, haya ni mambo ya kawaida

Ingawa mimi najua, ile dhiki unapata wewe

Hakuna asiyesumbuka, kama si leo labda ni kesho

Utulize usifanye kufa , maisha ndivyo yalivyo.

Hakuna kisokuwa, mwanzo wala na mwisho

Ebu fikiria, kabla shida ulikuwaje

Huu sio mwanzo, wala sio eti ni mwisho

Iko siku moja, utasahau yale ya jana.

Jema nd’o twaliomba, katika wakati huu

Stahimili fanya subira, kwani utafaulu

Mambo ni kwa mipango, yataka ufahamu

Furaha twaiomba, siku ikifika

2. Yote hayo majaribu, Mola mwenyewe anatambua

   Hata hivyo usife moyo, sio mwisho wa maisha yako

   Najua umejaribu, kwa mapenzi hata na riziki

   Bahati haijasimama, iko siku utafaulu.

   Kila jambo huenda, kwa hali ya mpangilio

   Dada vumilia, siku bado haijafika

   Siku ikifika, hata wewe utatambua

   Kwani mambo yote, sasa yatakamilika.

**8. KISULISULI**

1. Hiki ni kisulisuli, chenye upepo mkali

   Kinakuwa kwetu ni hatari, kila nikikifikiri

   Vile tuko mbalimbali, nakionea kisulisuli

2. Njoo tushirikiane, kabisa tusitengane

   Mola hakupanga, hivyo kamwe

   Uwe mwekundu mweusi, na hata uwe mweupe

   Lakini damu ni ile ile.

3. Tuliyonayo ni safari, na mbele ni kisulisuli

   Cha mabonde hata majabali, kuna upepo mkali

   Wavuma kila mahali, kutuletea kisulisuli x2

4. Kisulisuli kimeshanisonga, niliko na kule siko

   Hivi sasa kichwa chanizunguka,

   Kisulisuli niende wapi?

   Wewe na mimi tushirikiane

   Tukiweze kisulisuli x2

   Wewe na mimi tushirikiane

   Tuweze kisulisulix2

**9. JEMBE**

1. Alosema kwenye, vikoko hakuna wajenzi

   Alisema kweli, hata nami nampa pongezi

   Ninaye mwanangu, kwa jina yuaitwa Jembe

   Jembe mwana huyu, kwa kweli sijamuelewa

   Nilimpa shamba, apate kulipalilia

   Shamba la rutuba, tena kwa wingi wa mimea

   Siku za dhoruba, nipate kumsaidia

   Sina nijualo kumbe, shamba kalikimbia.

2. Jembe mwana, huyu yuko hapa tuliko leo

Kaliwacha shamba, na tumbili walichezea

Maskini najuta, shamba hilo kamuachia

Mate yadondoka, shamba zuri kama halua

Ila nikimuuliza, shamba kaliwacha na nani

Jembe hunijibu, ni matumbili na manyani.

Jembe urudi shambani (sirudi), hapa una kazi gani (sitaki)

Shamba sasa lina na nani (sijui), matumbili na manyani (pengine) } x3